SportPesa
TZS. 595,659,980
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Mwalimu** mkuu mbaroni madai kumpiga, kumvunja jino mwalimu mwenzake

UKURASA 3

# Nipashe

Jumatano Oktoba 20, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580739
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



**Ancelotti: Huyu Hazard sasa kachanganyikiwa**

UKURASA 21

# Dereva auawa jaribio kumpora silaha askari

UKURASA 2

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**
**BOMOABOMOA MACHINGA YACHUKUA SURA MPYA**
BOMOABOMOA ya vibanda vya wafanyabiashara wadogo, maarufu...

**UKURASA WA 4**
**TANZANIA, UFARANSA ZAJADILI USHIRIKIANO**
WATANZANIA wametakiwa kuchangamkia fursa ya ushirikiano wa...

**UKURASA WA 5**
**WAKILI KUTOA USHAHIDI KESI YA KUGHUSHI CHETI**
WAKILI wa kujitegemea Jerome Msemwa anatarajia kutoa ushahidi...


## Hatima ya kikokotoo cha mafao rasmi leo

UKURASA 3



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwahutubia baadhi ya waumini wa dini ya Kiislamu katika Baraza la Maulid, lililofanyika kitaifa viwanja vya Kaitaba, Bukoba Mjini, mkoani Kagera jana. **Picha zaidi Uk. 18. PICHA: OWM**

# Majaliwa: Serikali haina tofauti za kidini, kikabila

UKURASA 2

Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

**MICHEZO** SIMBA YAANIKA SIRI USHINDI GALAXY CAF UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Dereva auawa jaribio kumpora askari silaha

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Dar es Salaam, Ibrahim Said, mwenye umri kati ya miaka 30, amefariki dunia kwa madai ya kujaribu kupora silaha kutoka kwa askari polisi waliokuwa zamu katika kizuizi eneo la viwanda vidogo (SIDO) mjini hapo.

Said ambaye ni dereva wa kampuni ya Dangote inayozalisha saruji mkoani Mtwara, alikutwa na umauti usiku wa Oktoba 17, mwaka huu, saa 5:30 katika barabara kuu ya Kibiti - Lindi-Mingoyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP) Mtatiro Kitinkwi, alisema dereva huyo alikutwa na mauti kwa madai ya kutotii amri ya kusimama alipotakiwa na askari waliokuwa zamu katika kizuizi hicho.

Alisema dereva huyo akiwa na mwenzake (hakumtaja jina), alikuwa anaendesha lori la kampuni ya Dangote lenye namba za usajili T 992 DJZ lenye tela T 693 DKA.

Kamanda Kitinkwi alisema dereva huyo na mwenzake walipofika eneo hilo, askari waliwasimamisha kwa ajili ya ukaguzi lakini akakataa kutii amri.

"Huyu dereva aliposimamishwa na askari wetu waliokuwa zamu eneo lile, alikataa na badala yake akawa anampelekea gari kwa lengo la kutaka kumgonga," alisema Kitinkwi.

Kitendo cha askari kulikwepa lori hilo, alisema sehemu ya tela iligonga barabara na kwenda porini na kugonga mti, hivyo kusababisha hasara ya chombo husika kikiwemo kioo cha mbele.

Alisema baada ya lori hilo kugonga mti, Said alitelemka na kwenda kumvamia askari mwingine aliyekuwa na bunduki na kuanza kumchoma kisu sehemu mbalimbali za mwili wake kwa lengo la kutaka kumpora.

Kamanda Kitinkwi alisema kabla ya dereva huyo hajafanikiwa kuipora bunduki kutoka kwa askari huyo, wenzake aliokuwa nao zamu walimdhibiti na kupiga risasi hivyo kufariki dunia.

Alisema katika tukio hilo, ofisa mmoja na askari wawili waliumizwa na kupelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya sokoine kwa ajili ya kupatiwa matibabu. Pia alisema wanaendelea na uchunguzi kubaini iwapo Said alikuwa dereva halali wa kampuni hiyo.

Aliwataja waliojeruhiwa kuwa ni ACP Andrew Ngassa aliyelazwa wodi namba sita, Konstebo David Mbunda na Konstabo Denis Somanga, ambao wametibiwa na kuruhusiwa kurejea nyumbani.

Kaimu Mganga Mfawidhi Hospitali ya Sokoine, Dk, Dismas Mjarufu, alithibitisha kupokea majeruhi watatu ambao ni askari Polisi wakiwa na majeraha maeneo mbalimbali ya miili na mwili wa mtu mmoja aliyefariki dunia.

"Mpaka sasa yuko askari mmoja amelazwa chumba namba sita na wawili wametibiwa na kuruhusiwa kurejea nyumbani," alisema Dk. Mjarufu.

Dk. Mjarufu alisema majeruhi hao wamepata majeraha maeneo ya shingoni, mabegani na mikononi na kwamba hali zao zinaendelea vizuri.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi, akitia ubani kuashiria kuanza kwa Maulid ya kuadhimisha kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W), katika viwanja vya Maisara Suleiman, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja juzi usiku. **PICHA: IKULU**

## Wavuliwa uongozi tuhuma ubadhirifu

**Na Thobias Mwanakatwe**

VIONGOZI 18 wa vyama vya msingi vya ushirika, wilayani Maswa mkoani Simiyu wamevuliwa uongozi kutokana na tuhuma za ubadhirifu wa pesa za wakulima Sh. milioni 68 za msimu uliopita wa pamba.

Uamuzi huo ulichukuliwa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, wakati wa kikao cha wadau wa pamba wilayani humo, ambacho kilikuwa maalum kujadili mpango mkakati wa mkoa, katika kuongeza uzalishaji wa zao hilo, katika msimu wa 2021/22.

Mbali na kuwavua uongozi, Kafulila alitoa siku 14 kwa viongozi hao, ambao wanatuhumiwa, kuhakikisha ndani ya kipindi hicho, wanarejesha kiasi hicho cha pesa ambacho ni jasho la wakulima. Alisema serikali haiwezi kuvumilia kuwa na viongozi ambao wanahujumu zao la pamba ikiwamo kuwaibia wakulima.

Kafulila alimwagiza Ofisa Ushirika wilayani humo kuhakikisha anashughulikia kupatikana kwa viongozi wengine wapya kwa mujibu wa taratibu, ili shughuli za ushirika ziendelee na kuhakikisha fedha hizo za wakulima zinarejeshwa.

"Viongozi ambao siyo waadilifu hawana nafasi hata kidogo, tutachukua hatua kali kwa Amcos, ambazo zimekuwa na vitendo vya wizi kwa wakulima wake na hawa, ambao tumewasimamisha leo, wakishindwa kurejesha kwa siku hizo 14, watataifishwa mali zao," alionya.

Mkuu wa wilaya hiyo, Aswege Kaminyonge, alisema Bodi ya Pamba imeendelea kuleta mbegu kwa ajili ya wakulima, huku akibainisha shida ya kasi ndogo ya wakulima kununua mbegu. Alifafanua kuwa mahitaji ya mbegu za pamba wilayani mwake ni tani 3,000 na tayari wamepokea tani 700 tu.

# Majaliwa: Serikali haina tofauti za kidini, kikabila

**Na Lilian Lugakingira**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, imeonyesha kwa vitendo kuongoza taifa na kufikisha maendeleo kwa Watanzania wote bila kujali tofauti za kidini na ukabila.

Amesema serikali imeendelea kusimamia mshikamano, haki na umoja wa taifa, hivyo amewasihi Watanzania wote waendelee kumwombea Rais Samia ili aendelee kuiongoza vyema nchi.

Aliyasema hayo jana alipomwakilisha Rais Samia katika Baraza la Maulid lililofanyika kitaifa katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba mkoani Kagera.

Waziri Mkuu aliwataka waumini wa dini ya Kiislam nchini watumie maadhimisho hayo kama fursa muhimu kwao kuyasoma na kuyatafsiri kivitendo maisha ya Mtume Muhammad (S.A.W) katika mfumo wao wa maisha ya kila siku.

"Tafakuri hiyo ituwezeshe kuishi maisha ya undugu, kupendana, kuheshimiana na kushikamana miongoni mwetu Waislam pamoja na Watanzania wote kwa ujumla," alisema.

Majaliwa alisema amani ni tunu adhimu ambayo Mwenyezi Mungu ameikirimia Tanzania, akifafanua: "Kudumisha amani iwe ni wajibu wa kila mmoja wetu kwani amani ndiyo kila kitu.

"Bila amani hatuwezi kupata maendeleo, hatuwezi kufanya ibada, watoto wetu hawawezi kwenda shule na mambo mengine mengi," alisema.

Aliongeza kuwa Tanzania imekuwa kinara katika kuenzi na kudumisha amani, hivyo ni wajibu wa kila Mtanzania kuendelea kuitunza amani hiyo kwa kuwafundisha vijana na watoto misingi ya amani ili nao waidumishe.

"Serikali inatambua umuhimu wa madhehebu ya dini katika kudumisha amani. Viongozi wa dini mmekuwa mabalozi wema na kudumisha amani yetu kwa miongo kadhaa. Jitihada zenu zote zimewezesha nchi yetu kupata utulivu kila wakati na kuwa kimbilio la majirani pindi wanapopata machafuko," alisema.

Majaliwa alitumia fursa hiyo kuwaomba viongozi wa dini kuwaelimisha waumini wao kufanya maandalizi kwa ajili ya kushiriki katika sensa ya watu na makazi ambayo inatarajiwa kufanyika Agosti mwakani.

"Zoezi hili litaiwezesha nchi kupata takwimu za msingi zinazotumika katika kutunga sera, kupanga mipango na programu za maendeleo pamoja na kufuatilia utekelezaji wake," alisema.

Waziri Mkuu pia alitumia fursa hiyo kuwasisitiza wananchi kujitokeza kwa wingi kwenda kupata chanjo ya kujikinga na Uviko-19.

"Suala la afya ni muhimu na si la kufanyia maskhara. Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Samia ameshazindua kampeni ya chanjo dhidi ya Uviko-19. Tumuunge mkono," alisema.

Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeir bin Ally, aliwasihi wananchi waendelee kuwaheshimu na kuwatii viongozi wao wa dini na serikali kwa kuwa hiyo ndiyo tabia njema ambayo inachangia taifa kuwa na maendeleo.

Katibu Mkuu wa BAKWATA, Sheikh Nuhu Jabir, aliipongeza serikali kwa namna inavyowahudumia wananchi kwa kutoa takribani Sh. trilioni moja kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo.

## HABARI KITAIFA

# Hatima kikokotoo cha mafao leo

**Na Romana Mallya**

WAKATI baadhi ya vyama vya wafanyakazi vikisisitiza hakitaki kikokotoo kipya cha mafao ya wastaafu, leo serikali inatarajiwa kutoa taarifa kuhusu suala hilo.

Jumamosi Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kupitia Kaimu Rais, Dinnah Masamani, kilitangaza msimamo wake kuhusu malipo ya mafao ya wastaafu katika kada mbalimbali nchini, ikiwamo walimu, kikisisitiza kuendelea na kikokotoo cha sasa.

Nipashe jana ilimtafuta Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira na Uratibu, Agustino Tendwa, kupata ufafanuzi kuhusu hatua iliyofikiwa na kamati iliyoundwa na serikali kushughulikia suala hilo miezi mitano iliyopita.

"Kama unavyosema, ni kweli kuna kamati iliundwa, na Rais aliyeondolewa CWT anajua hilo. Msisikilize upande mmoja, Mheshimiwa Waziri (Jenista Mhagama) atatoa taarifa kesho (leo)," alisema.

Oktoba 20, 2017, Bunge lilipitisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambayo mbali na kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na kufanya marekebisho kwenye Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), kanuni zake ziliweka utaratibu wa kulipa mafao kwa mkupuo kwa asilimia 25 na asilimia 75 iliyobaki kulipwa kama mshahara kwa mstaafu kwa miaka 12.

Sheria hiyo ambayo pia iliweka umri wa kustaafu kuwa miaka 55 kwa hiari na miaka 60 kwa lazima (kwa kada maalum kama vile madaktari na maprofesa umri wa kustaafu ni miaka 65 kwa lazima), iliibua mjadala mkali kitaifa uliosababisha Rais John Magufuli kuingilia kati, akaagiza kikokotoo hicho kipya kianze kutumika mwaka 2023.

Ikirejewa msimamo wao wa CWT uliotangazwa na Dinnah Jumamosi mkoani Mtwara alipozungumza na wajumbe wa Kamati ya Baraza la Mkoa wa CWT Mkoa wa Mtwara, chama hicho kinaamini kikokotoo kipya kilichopendekezwa na serikali kilionekana kutokubalika kwa wadau wengi hadi ilipoamuliwa kisitishwe kwa ajili ya kuwapa nafasi wadau kujadili faida na hasara zake.

"Suala hili lilikuja juu miaka iliyopita na ilionekana halifai, ukatolewa muda mpaka mwaka 2023 kuendelea na kikokotoo kilichopo kwa lengo la kutoa muda wa majadiliano, lakini sisi CWT tunatamani kuendelea kutumia kikokotoo cha zamani, hatutaki kiwe na kikomo," alisema.

Alisema CWT inaona kikokotoo kipya hakiwatendei haki wafanyakazi kwa kuwa ni muhimu anayestaafu apewe fedha zake zote kwa ajili ya kufanikisha mipango yake ya maisha baada ya kutoka katika utumishi wa umma.

"Lakini sisi kama chama tuongee, tusiongee kwa kuwa muda wa mpito unakaribia kuisha, msimamo wetu ni kuona kile kikokotoo cha zamani kinaendelea kuwapo, hatuhitaji kuwekewa mafao yetu kidogo kidogo.

"Hiyo miaka 60 kwa sasa tunafika kwa neema ya Mungu, watupe mzigo wetu tufe nao kibindoni," alisema.

## Bomoabomoa machinga yachukua sura mpya

**Na Maulid Mmbaga**

BOMOABOMOA ya vibanda vya wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, imeendelea kwenye maeneo yaliyokatazwa mkoani Dar es Salaam licha ya uongozi wa mkoa huo kuongeza siku 12 kwa kundi hilo kuyapisha maeneo hayo.

Juzi, Mkuu wa Mkoa huo, Amos Makalla, alitangaza kuongeza siku 12 kwa wafanyabiashara hao kuondoka kwenye maeneo yasiyo rasmi na kuutumia vizuri muda huo ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza muda utakapoisha.

Hata hivyo, Nipashe ilishuhudia jana kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa huo vibanda vya machinga vikionekana kubomolewa.

Maeneo kulikoshuhudiwa ubomoaji ni pamoja na Tabata, Segerea, Mwenge, Mlimani City, Tegeta, Makumbusho, Temeke, Mbagala, Posta, Gongolamboto, Buguruni na Vingunguti. Upangaji wa machinga ni moja ya mipango na mikakati ya Makalla aliyoanza kuitekeleza Agosti mwaka huu. Alisema amedhamiria kuufanya mkoa huo kuwa safi na kurejea katika hadhi yake ya kibiashara.

Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Jumanne Shauri, aliiambia Nipashe kuwa wameweka mikakati ili kuhakikisha maeneo yote yaliyosafishwa yanabaki safi na kutoruhusu mtu yeyote kurudi.

Alisema mikakati yao inajumuisha kuweka utaratibu wa kupitisha doria mara kwa mara ili maeneo hayo yawe wazi.

Alibainisha kuwa baadhi ya maeneo watu wanaonekana kuondoa vibanda lakini wanaendelea na biashara kwa kuweka mwavuli, jambo ambalo alisisitiza kwamba haliruhusiwi.

Alisema machinga wote wanatakiwa kwenda maeneo waliyopangiwa na yeyote atakayekaidi, atakamatwa na kufikishwa Mahakama ya Jiji na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.



Mwonekano wa barabara ya Nyerere katikati ya Jiji la Mwanza, iliyokuwa imefurika machinga na kusababisha watu pamoja na magari kushindwa kupita, ikiwa wazi kwa sasa, baada ya serikali kuwahamishia kwenye maeneo rasmi. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Mwalimu mkuu matatani madai ya kumpiga na kumng'oa jino mwalimu

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

JESHI la Polisi, mkoani Morogoro linamshikilia Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mkuyuni, wilayani Morogoro, Musa Hasira (46), kwa tuhuma za kumshambulia kwa fimbo na kumng'oa jino mwalimu mwenzake wa kike.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Fortunatus Musilim, amethibitisha kushikiliwa kwa Mwalimu Hasira, akituhumiwa kumshambulia kwa fimbo sehemu mbalimbali za mwili, Witness Makoti (31) kutokana na sababu ambazo hazijajulikana.

Kamanda Musilim alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Oktoba 15, mwaka huu, majira ya saa 6:00 mchana.

Alisema mtuhumiwa alimvamia mwalimu huyo na kupiga kwa kutumia fimbo, ngumi na makofi katika sehemu mbalimbali za mwili hatua iliyomfanya Makoti apige kelele na mwalimu mwingine kujitokeza kumsaidia.

Musilim alisema chanzo cha tukio hilo bado kinachunguzwa na kwamba Mwalimu Makoti tayari amepatiwa matibabu katika Zahanati ya Mkuyuni na kuendelea kuuguza majeraha yake akiwa nyumbani.

Diwani wa Mkuyuni, Mwinyi Bui, akizungumza kwa njia ya simu, alisema kwa taarifa alizopata ni kuwa Mwalimu Makoti alishambuliwa wakati akiwa darasani na wanafunzi watatu wa kike wakijadiliana maswala ya masomo.

Alibainisha kuwa baada ya kuokolewa na mmoja wa walimu wenzake, walikwenda kuripoti kituo cha Polisi Mkuyuni na kupewa fomu namba tatu ya polisi (PF3), ili aende kutibiwa katika zahanati hiyo na baadaye hospitali ya Nunge, ambako waligundua Mwalimu Makoti alipata vidonda mdomoni na kuvunjika jino.

Diwani huyo alisema kwa sasa Makoti amekuwa na hofu juu ya usalama wake kama mtuhumiwa ataachiwa huru, hivyo kuiomba serikali na jamii anapofanya kazi na kuishi kumsaidia, ili haki itendeke baada ya tukio hilo.

Bui alisema baada ya kutokea kwa tukio hilo, viongozi mbalimbali wa wilaya, tarafa, kata na vijiji wamekutana kwa vikao vya mara kwa mara kujadili suala hilo.

Alisema shuleni hapo kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wanafunzi na walimu kuwa mwalimu mkuu huyo amekuwa na tabia zisizoeleweka kwa wanafunzi wa kike na wanapotoa taarifa kwa walimu wamekuwa wakifumbia macho.


**KUPOTEA KWA VYETI**



**FREDNAND ZEBEDAYO NYANDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne Chenye index namba **S.1986-0041 Igokelo Sekondari mwaka 2009. Cheti cha Chuo (VETA) namba 13/CBA-II/MVM/15D/250 cha Kalwande Church Service and Training Centre Mwanza mwaka 2015. Cheti cha chuo (VETA) namba 13/CBA-III/MVM/16D/004 cha Kalwande Church Service and Training Centre Mwanza mwaka 2016. Cheti cha JKT namba 367965 831 KJ Mgulani mwaka 2020. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/URA/RB/493938/2021.**

# Gwajima awataka diaspora kushiriki fursa kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu,**
ST. PETERSBURG

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amewataka Watanzania wanaoishi na kusoma nchini Urusi kutumia fursa zilizoko Tanzania katika kuwekeza na kuwasaidia wananchi.

Dk. Gwajima aliyasema hayo jana jijini hapa alipokutana na kufanya mazungumzo na Watanzania wanaoishi na wanaosoma katika vyuo mbalimbali.

Alisema Tanzania ina fursa nyingi za kuwekeza katika sekta mbalimbali ili kusaidia jamii zikiwamo afya, utalii na madini ambazo zinaweza kuchangia katika maendeleo ya taifa.

Waziri alisema kuishi au kusoma nje ya Tanzania hakufungi milango kuwekeza nyumbani na kuleta mabadiliko katika taifa alilotoka mtu lakini ndilo linaongeza fursa na nafasi ya kuleta mabadiliko katika jamii kutokana na mambo mapya ya kujifunza kutoka mataifa mengine.

"Niwaambie ndugu zangu nyumbani kumenoga wekezeni nyumbani. Haijalishi wewe unaishi huku au wewe ni mwanafunzi, mnaweza mkajiunga pamoja na kuanzisha umoja wenu mkatafuta wafadhili mkiwa Urusi na mkawasaidia Watanzania wenzenu," alisema Waziri.

Pia alisisitiza kuwa serikali ya Tanzania iko pamoja na Watanzania wanaoishi na kusoma nje ya Tanzania kwa kuwa azma ya serikali ni kuweka mazingira rafiki katika kuhakikisha wanapata fursa za kuchangia katika maendeleo ya taifa huko huko waliko ikiwamo kuwekeza katika sekta mbalimbali nchini.

Kaimu Balozi wa Tanzania nchini Urusi, Dk. Switbert Mkama, alimhakikishia Dk. Gwajima kushirikiana na Watanzania wanaoishi na kusoma nchini hapa kupata fursa zilizoko Tanzania katika kuwekeza na kusaidia jamii katika sekta mbalimbali.

"Mheshimiwa Waziri tutawashika mkono hawa wenzetu huku na kuwapa taarifa za fursa zilizoko nyumbani ili watoe mchango wao katika maendeleo ya taifa letu hata wakiwa nje ya Tanzania," alisema Mkama.

Naye Mkurugenzi na Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO), Vickness Mayao, alisema inawezekana kwa Watanzania wanaoishi na kusoma nje kujipanga na kufungua asasi za kiraia nchini.

Mayao alisema taratibu zinaruhusu kuanzishwa kwa NGO za kimataifa nchini na kuwataka kuchangamkia fursa hiyo katika kuhakikisha wanatumia fursa ya kuwa nje ya Tanzania kusaidia jamii.

Akizungumza kwa niaba ya Watanzania wanaoishi na kusoma nchini Urusi, Lucas Muchunguzi, aliishukuru serikali ya Tanzania chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwawezesha Watanzania kupata fursa za kusoma nje ya nchi na kuahidi kutumia uzoefu na elimu watakayoipata kusaidia kuleta mabadiliko na kuchangia katika maendeleo ya taifa.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima (kushoto), akifurahia zawadi kutoka kwa wanafunzi wanaosoma nchini Urusi, wakati alipokutana nao pamoja na Watanzania wanaoishi nchini humo, baada ya kumalizika kwa kongamano la wanawake aliloshiriki akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: WIZARA YA AFYA**

# Wapanga foleni huduma ya choo

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WANAFUNZI wanaosoma katika Shule ya Sekondari Mazinge, Manispaa ya Shinyanga, wamedaiwa kupanga foleni wakati wa kujisaidia kutokana na upungufu wa matundu ya vyoo.

Mkuu wa Shule hiyo, James Msimba, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki kwenye mahafali ya kidato cha nne katika shule hiyo.

Alisema shule hiyo inakabiliwa na upungufu wa matundu ya vyoo kutokana na kuwa na matundu sita, manne yanatumiwa na wasichana na mawili wavulana, hivyo kusababisha wanafunzi kupanga foleni wakati wa kujisaidia.

"Shule ina wanafunzi 778 hivyo matundu sita ya choo hayatoshi kwao kuwahudumia. Inatakiwa angalau tuwe na matundu 10 ndipo yatakidhi mahitaji ya wanafunzi waliopo," alisema Msimba.

"Tunaiomba serikali pamoja na wadau watusaidie kutatua baadhi ya changamoto ambazo zinatukabili shuleni hapa ikiwamo upungufu huu wa matundu ya choo," aliongeza.

Naye mgeni rasmi katika mahafali hayo, Meneja Miradi kutoka Shirika la Rafiki, Ahsante Nselu, ambao wanajishughulisha na masuala ya kijamii na aliahidi kutatua baadhi ya changamoto shuleni hapo.

Katika hatua nyingine, Meneja huyo aliwataka wazazi mkoani Shinyanga kutenga muda wa kulea watoto katika malezi bora badala ya kujishughulisha muda wote na maisha, hali ambayo inasababisha mmomonyoko wa maadili kwa wanafunzi.

# Tanzania, Ufaransa zajadili ushirikiano kiteknolojia

**Na Salome Kitomari**

WATANZANIA wametakiwa kuchangamkia fursa ya ushirikiano wa kiteknolojia kati ya Tanzania na Ufaransa kwa kutumia magari ya mfumo wa umeme unaotunza mazingira.

Waziri wa Mambo ya Nje, Biashara na Vivutio vya Kiuchumi wa Ufaransa, Franck Reister, alisema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari katika ofisi za ubalozi wa nchi hiyo Dar es Salaam baada ya kupanda na kutembea kidogo kwa magari yanayotumia umeme yanayomilikiwa na kampuni ya utalii ya Mount Kilimanjaro Safari Club.

"Ni furaha kubwa kuwapo nchini na kupanda gari linalotumia umeme ambalo limezalishwa na kampuni ya Ufaransa. Ni gari la maisha kwa kuwa linatumia umeme na halina madhara kwenye mazingira, hakuna hewa ukaa na kelele zinazoharibu mazingira," alisema.

Reister alisema magari hayo ni mazuri kutumika kwenye hifadhi na maeneo ya utalii ambayo wanyama hawapendi kelele au usumbufu na yanaweza kutumika kwenye vyombo vya usafiri wa umma ili kupunguza uharibifu wa mazingira.

"Tunafarijika kushirikiana na kampuni za kitanzania, Chuo cha Ufundi Arusha na vyuo vingine. Tunaamini katika ubunifu na kujenga maendeleo endelevu kwa ajili ya Watanzania na ni mfano mzuri kwa maisha ya baadaye kwa kuwa ni rafiki kwa mazingira," alisema Reister.

Alisema kwa sasa serikali ziko katika hatua mbalimbali za majadiliano ya namna kampuni za nchi hizo zitakavyoshirikiana lakini lengo kubwa ni kushirikisha teknolojia.

Naye Mwakilishi wa Kampuni ya Mount Kilimanjaro Safari Club, George Olemeng'arai, alisema wanatumia magari ya mfumo wa umeme kwa zaidi ya miaka tisa ambayo yanatumika kutembeza watalii eneo la Gurumet na Hifadhi ya Taifa Serengeti tangu mwaka 2017.

"Tumebadili kutokana na mahitaji ya dunia kwenda kwenye magari ya umeme yanayotunza mazingira kuondoa hewa ukaa na kelele kwa kuwa injini yake haina kelele. Mafuta yanapanda kila wakati, ukitumia gari hili unaokoa fedha," alisema.

Pia alisema wanyama hawataki kelele na kwamba wanayatumia magari hayo kwa safari za utalii na kwamba betri yake inakwenda umbali wa zaidi ya kilomita 130 na kuhitaji kuchajiwa na gari linaweza kwenda kwa mwendo wa 130 kwa saa.

Waziri huyo alikuja nchini na ndege ya kampuni ya Air France moja kwa moja kutoka Paris, Ufaransa hadi Zanzibar. Ndege hiyo ilikuwa na wageni wengine ambao watatumia muda wao kwenye vivutio mbalimbali nchini.

Pia amekutana na mawaziri mbalimbali nchini kujadili namna ya kuendelea kushirikiana na pia alikutana Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

HABARI KITAIFA

# Wakili kutoa ushahidi kesi kughushi cheti

**Na Kulwa Mzee**

WAKILI wa kujitegemea Jerome Msemwa anatarajia kutoa ushahidi katika kesi ya kughushi cheti cha ndoa, inayomkabili Khairoon Jandu, Novemba Mosi, mwaka huu.

Kesi hiyo inasikilizwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele Hakimu Mkazi Mwandamizi Joseph Lwambano na juzi, ililetwa kwa ajili ya usikilizwaji, lakini ilikwama kwa sababu wakili wa mshtakiwa huyo Abubakar Salim, alikuwa na udhuru.

Kwa mujibu wa taarifa iliyofikishwa mahakamani hapo, wakili huyo alikwenda kuhudhuria kesi, Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi.

Wakili wa serikali Ashura Mzava alimlalamikia wakili huyo wa utetezi akidai ni mara ya tano sasa kesi hiyo, imeshindwa kuendelea kutokana na yeye kutofika mahakamani.

"Mheshimiwa hakimu pamoja na wakili kuleta taarifa hii, lakini naona kama kuna mchezo anafanya, hii ni mara ya tano sasa kesi imeshindwa kuendelea kwa yeye kutofika mahakamani, aseme basi ni tarehe zipi atakuwapo mahakamani mimi naandaa mashahidi, lakini wakili haonekani mahakamani," alidai Wakili Mzava.

Baada ya kueleza hayo, mshtakiwa Khairoon alieleza mahakama kuwa wakili wake amesema atafika mahakamani Novemba mosi, pili na tatu.

Hakimu Luambano alisema kesi hiyo itaendelea kusikilizwa mfululizo katika tarehe hizo na kumtaka mshtakiwa Khairoon amweleze wakili wake afike mahakamani, bila kukosa katika tarehe zilizopangwa.

Mahakama ilimuonya shahidi namkumtaka pia afike mahakamani Novemba mosi, mwaka huu.

Katika kesi hiyo, Khairoon anadaiwa kuwa katika tarehe na mwezi usiofahamika mwaka 2020, ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam, kwa nia ovu, alighushi cheti cha ndoa.

Ilidaiwa kwamba alighushi cheti hicho akionesha kuwa ni halali kimetolewa na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), wakati akijua si kweli.

Katika shtaka la pili, inadaiwa mshtakiwa huyo alighushi cheti cha kuzaliwa cha Gurditsingh Jandu akionesha ni halali kimetolewa na RITA wakati akijua si kweli.

# TASAF yaahidi matumizi mazuri fedha UVIKO-19

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Ladslaus Mwamanga, amesema wamejipanga kuhakikisha kwamba utekelezaji wa miradi ya ajira za muda kwa walengwa wa mpango wa kunusuru kaya masikini unaanza haraka.

Hatua hiyo inakuja baada ya mfuko kupokea fedha ambazo serikali imeugawia kwa ajili ya kusaidia kaya hizo.

Tayari serikali imeiidhinishia TASAF Sh.bilioni 5.5 kati ya fedha zilizotolewa kwa mkopo wenye masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mwamanga alisema wanamhakikishia Rais Samia Suluhu Hassan kwamba utekelezaji wa miradi kupitia fedha hizo wataufanya kwa wakati kama ambavyo wameelekezwa.

"Natoa shukrani zangu za dhati kwa Rais Samia, kwa kufanikisha upatikanaji wa fedha hizi ambazo zitaharakisha maendeleo katika sekta mbalimbali na kwa kutambua kuwa Watanzania wenzetu wanaoishi katika mazingira duni na kuwatengea Sh.bilioni 5.5 zitakazoimarisha ustawi wao ambao uliyumba kutokana na ugonjwa wa corona,"alisema Mwamanga.

"Tunamhakikishia kwamba utekelezaji wa miradi utafanywa kwa wakati na hakuna fedha zitakazotumika nje ya malengo yaliyokusudiwa."

Mwamanga alisema fedha hiyo ambayo serikali imetoa kwa ajili ya mpango wa TASAF ni kielelezo tosha kwamba inajali wananchi wake hususani wale wanaoishi katika mazingira duni.

"Na kupitia fedha hizi ambazo serikali imeiidhinishia TASAF kwa ajili ya walengwa, tunaahidi tutatekeleza miradi ya ajira ya muda itakayochangia kuongeza upatikanaji wa chakula na kuboresha huduma katika sekta za afya, elimu, maji na hifadhi ya mazingira kwa hizi kaya lengwa,"alisema Mwamanga.

"Kwa kuwa muda wa matumizi ya fedha hii umewekwa bayana, menejimenti ya TASAF kwa muongozo wa kamati ya uongozi ya taifa, itahakikisha maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya ajira za muda kwa walengwa katika maeneo yatakayoidhinishwa unaanza haraka mara tu baada ya fedha kupokelewa. Usimamizi utafanyika kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa viwango na thamani ya fedha."


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII TASAF**

## TAARIFA KWA UMMA

### UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19 KWA MPANGO WA KUNUSURU KAYA ZA WALENGWA WA TASAF

TASAF inatekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya za Walengwa katika Halmashauri 184 za Tanzania Bara, Unguja na Pemba. Idadi ya walengwa wa TASAF ni takriban kaya milioni 1.4 zenye watu wanaokadiriwa kufikia milioni 10. Walengwa hawa wanatoka katika kaya zinazoishi katika mazingira duni na hivyo kupatiwa ruzuku ya kujikimu, kufanya kazi kwenye miradi ya jamii na kulipwa ujira ambao unaongeza pato kwenye kaya na kuunganishwa katika vikundi vya kuweka akiba na kuwekeza ili kukuza uchumi wa Kaya. Mara baada ya uzinduzi wa kipindi cha Pili cha Awamu ya Tatu ya TASAF mnamo Februari 2020, nchi yetu ilipata janga la UVIKO 19 na shughuli za mikusanyiko zilisimamishwa ili kuzuia maambukizi ya homa ya mapafu. Utekelezaji wa shughuli za Mpango ambazo hukutanisha walengwa na wataalam ili kutoa elimu kuhusu lishe, ufugaji, kilimo, na ujasiriamali nazo zilisimama. Walengwa hawakupata fursa ya kukutana wao kwa wao au na wataalam ili kubadilishana uzoefu na kupata maarifa mapya ili kuboresha utendaji wao katika uzalishaji.

Athari za UVIKO 19 zilianza kujitokeza mara baada ya shughuli za kijamii kurejea kama kawaida. Walengwa ambao ni kaya zinazoishi katika mazingira duni walikuwa wamerudi nyuma kiuchumi na walipoteza rasilmali zao kama mifugo kwa kuziuza ili kupata fedha ya kujikimu. Kufuatia hali hii, Serikali iliweka mikakati mbali mbali ya kunusuru kaya hizi. Moja ya mikakati iliyowekwa ni kutafuta fedha na kutoa ruzuku kwa kaya hizi ili kukabiliana na athari zilizotokana na UVIKO 19.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepata Mkopo wenye masharti nafuu wa Dola za Kimarekani Milioni 567 sawa na shilingi trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha Kimataifa (IMF) kwa ajili ya Kampeni ya Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19. Kati ya fedha hizo, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF umeidhinishiwa shilingi bilioni 5.5 (US$ milioni 2.4).

Fedha hizo zitatumika kulipa ujira kwa kaya za walengwa ambao watatekeleza miradi ya jamii. Kupitia program ya ajira za muda kwa walengwa, jumla ya kaya za walengwa 40,740 zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi wanaoishi katika maeneo ya mjini, watatekeleza miradi ya jamii ambayo itachangia kuongeza upatikanaji wa chakula na kuboresha huduma katika sekta za afya, elimu, maji na hifadhi ya mazingira.

Walengwa watafanya kazi kwa muda wa miezi mitano na kulipwa wastani wa shilingi 135,000 kwa kaya. Fedha hizi zitalipwa ndani ya mikupuo mitatu kwa mujibu wa kalenda ya malipo kwa walengwa. Fedha watakazolipwa walengwa zitatumika kufufua au kuimarisha biashara zao ambazo zilizoathirika zaidi kutokana na UVIKO 19. Pamoja na ajira za muda, walengwa hawa wa mijini wataendelea kupokea ruzuku za msingi za kila baada ya miezi miwili ambazo wanaendelea kulipwa hata sasa.

Ili kuendana na matakwa ya kutumia fedha hiyo ndani ya kwa kipindi cha miezi tisa, Menejimenti ya TASAF kupitia Kamati ya Taifa ya Uongozi, itahakikisha maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya ajira za muda kwa walengwa katika maeneo yatakayoainishwa unaanza mara tu baada ya fedha kupokelewa. Usimamizi utafanyika kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa viwango na thamani ya fedha. Ni matumaini yetu kwamba fedha hii iliyotengwa kwa ajili ya TASAF itasisimua uchumi wa kaya uliokuwa umedorora kutokana na athari za UVIKO-19 na hivyo kuchangia katika mapambano ya kuondoa umaskini ambayo ni sehemu ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa.

TASAF inatoa shukurani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kutambua kuwa Watanzania wanaoishi katika mazingira duni wameathirika kiuchumi na UVIKO 19 na hivyo kuwatengea shilingi bilioni 5.5 zitakazoimarisha ustawi wao. Utekelezaji wa miradi utafanywa kwa wakati na hakuna fedha itakayotumika nje ya malengo yaliyokusudiwa.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF**
**S. L. P. 2719 Dodoma**

216520601

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wamachinga mkubali kuhama bila shuruti

**KWA** muda mrefu, wafanyabiashara wadogo maarufu kama 'machinga' wamekuwa wakifanya biashara zao katika maeneo mbalimbali nchini, yakiwamo yasiyo rasmi kama kandokando ya barabara, na kusababisha kero kwa watumiaji wa barabara na uchafuzi wa mazingira.

Hali hiyo imeifanya serikali kuchukua hatua za kutaka kuhakikisha wanafanya biashara zao katika mazingira rafiki ambayo watakuwa salama na pia kutochafua mazingira na kuhatarisha afya zao. Kinachoendelea mkoani Dar es Salaam sasa ni kuwaondoa katika maeneo waliopo na kwenda katika maeneo yakiwamo masoko waliotengewa ili barabara ziwe wazi, lakini wasichafue mitaro ya kupitisha maji ya mvua.

Kwa kuwa hatua hizo za serikali zina nia nzuri kwa ajili yao, wito wetu kwa wamachinga ni kwamba, wazingetia maelekezo ambayo wamepewa ya kuhama ili yafanyike bila shuruti wala mvutano. Tunashauri hivyo, kwa sababu uzoefu unaonyesha kuwa kila wamachinga wanapohamishwa, huwa kunatokea mvutano kati yao na vyombo vya dola, jambo ambalo kwa upande wetu tunaona si jema.

Tumeshaanza kuona baadhi yao wakifanya ukaidi wakutekeleza maelekezo ya kuondoka katika maeneo yasiyoruhusiwa. Baadhi wanavunjiwa vibanda, lakini kesho yake wanarejea kwa kupanga bidhaa zao. Serikali ina nia njema ya kutaka wamachinga waendeshe shughuli zao katika maeneo ambayo ni rasmi.

Limekuwa ni jambo la kawaida katika miji kukuta wamepanga bidhaa zao kando ya barabara na kusababisha kero kwa wapita njia, lakini kuhatarisha usalama wao.

Kwa machinga wa Dar es Salaam, Oktoba 18, mwaka huu, ilikuwa mwisho wao kufanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi, lakini Mkuu wa Mkoa huo, Amos Makalla, juzi alitangaza kuwaongezea siku nyingine 14 za kujiandaa kuhama.

Wiki hii, akihutubia wakazi wa Jiji la Arusha, Rais Samia Suluhu Hassan, aliipongeza Dar es Salaam kwa kuwapanga machinga na kuwezesha maeneo mengi kuonekana vizuri na kurahisisha usafi. Rais anataka miji na majiji mengine kuiga mfano huo ulioonyeshwa na wenzao wa Dar es Salaam. Na hili tunaona ni muhimu wadau wote kuhusika, kuanzia viongozi hadi machinga wenyewe kushirikiana katika hili.

Tunatambua na kuthamini shughuli za machinga, kutokana na ukweli kwamba wamekuwa na mchango mkubwa kwa watu wengi kujiajiri na kujiingizia kipato cha kuendesha maisha yao ya kila siku, huku wakilipa kodi za serikali.


Lakini ni vyema biashara zao zikafanyika katika mazingira ya usafi na usalama kuliko ilivyo sasa, ambapo wengi wao 'wanavamia' hata maeneo yasiyo rasmi na kusababisha usumbufu kwa wengine. Jambo lingine ambalo hujitokeza, ni pale mpita njia anapogusa bidhaa zao, hutolewa matusi mazito yakiwamo ya nguoni, na wengine kudiriki kuwapiga baadhi ya watu kwa kukanyaga bidhaa hizo.

Kwa mazingira kama haya, tunaamini kwamba, hatua zinazochukuliwa na serikali za kuwahamisha kutoka kwenye maeneo yasiyo rasmi, zitapunguza kero mbalimbali zinazosababishwa na wafanyabiashara hao. Rais ameagiza uhamishaji wa machinga ufanyike kistaarabu, na ndivyo tunaona ikifanyika, na matarajio yetu ni kwamba kila kitu kiende sawa, hatimaye maisha yaendelee kama kawaida.

Hata hivyo, tunasisitiza kwamba wamachinga wanawajibika kuheshimu maagizo na maelekezo ya serikali kwa kukubali kuyahama maeneo yaliyokatazwa bila shuruti, kwa kuwa kufanya hivyo ni kutaka kupimana ubavu na serikali, kitu ambacho hawataweza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mkutano msajili, vyama uwe mwanzo mzuri wa demokrasia

Na Ani Jozeni

**JUHUDI** za kurudisha maisha ya kidemokrasia katika siasa yanaanza kupiga hatua kwa kiwango, kwanza kutokana na kuondolewa hofu iliyokuwapo awali hasa katika uhuru wa kujieleleza.

Kinachojiri ni wadau walipoanza kuutumia uhuru huo katika maeneo tofauti na mtafaruku ukazuka.

Ndiyo jitihada za kuondoa mtafaruku huo zikaanza, kuhakikisha kuwa uhuru wa kujieleza na kufanya mikutano ya kisiasa kwa kiwango fulani unathibitishwa, hata hivyo bado upo wasiwasi ni kwa kiwango gani jambo hilo linaweza kufaulu na uhuru huo ukaendelea.

Ni suala la kujipanga kwa pande zinazohusika, walio madarakani hii ni pamoja na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, inataka nini, na vyama pia hitaji lao ni nini?

Ukiangalia suala hilo unakuta ni jambo la kimfumo, kutokana na mazoea yaliyokuwamo wakati wa awamu ya tano, ambayo baadhi ya walioko madarakani, wanaona ndiyo hali ya kawaida.

Wale wenye hisia ya demokrasia wanaona kuwa hali hiyo si njema, kunatakiwa uhuru wa kujieleza na kukutana uwepo wa vyama vijipambanue na kueleza sera zake.

Hata hivyo hofu inabaki kuwa hali hiyo isipodhibitiwa inaweza kuanza kuvuruga amani.

Halafu wanaohitaji uhuru huo wana malengo yao, na mbinu zao za kufikia matamanio hayo, wakipata mwanya huutumia kikamilifu.

Hapo ndiyo kuna tatizo, kuwa uhuru wa kujieleleza na kukutana na uwepo ila usiharibu amani ya nchi ambayo ina maana kuwa ajenda kubwa ya upinzani, ya kutaka kuandikwa katiba mpya, isiwepo.

Labda tatizo liko katika suala la hayo mazoea, kuwa kwa baadhi ya watawala kutaja katiba mpya inakuwa ni kama kuwataka watu waasi uongozi wa serikali iliyopo madarakani, wakati ni mada ya kawaida ya kujipigia debe itumike wakati ukifika.

Watanzania walishaona wimbi la kutaka katiba mpya awali, lilivyoingizwa katika mchakato, hadi kumalizika, lakini bila kupatikana kile kilichokuwa kimekusudiwa.

Kwa maana hiyo yako masuala kadhaa ya kujadili kuhusu dai hilo la katiba mpya, kama kuna haja ya kuchelea majadiliano wakati inajulikana kuwa chama tawala kikisema katiba iliyopo inatosha, kinaweza kupata kura za kutosha kwa mpangilio huo, na bila vurugu.

Kwa maana hiyo kuna woga au hofu ya kubadilisha mazingira ya kujieleza kisiasa, ili yaendane na zama mpya za kutaka uwapo halisi wa demokrasia ya vyama vingi.

Vipo vyama vimejitokeza kumsikiliza Msajili wa Vyama vya Siasa, na si ajabu akaandamana na wadau wengine serikalini, kwani walitajwa mwanzoni kuwa wangekuwepo pia.

Kimsingi, huwezi kusema kuwa kutofika kwa baadhi ya vyama vya siasa kunatokana na ukali wa misimamo yao kwani inavyoelekea upana wa uhuru wa kujieleza uliotolewa hadi sasa haukidhi hitaji la kufanya 'siasa.'

Hata hivyo, endapo wigo huo ungepanuliwa ikawa ni pamoja na kufuatilia mjadala wa katiba mpya unaofuatiliwa na sehemu isiyo ndogo ya wataalamu, washauri na hata viongozi wa baadhi ya makundi ya kijamii ingesaidia. Huwezi kufanya siasa endapo hutaweza kutoa ya moyoni na ukawa huru kusema na mengineyo.

Ina maana kuwa mkutano unaotarajiwa wa Msajili wa Vyama vya Siasa na sehemu kubwa ya vyama vya siasa iweke msingi wa kupanua kwa mjadala wa kisiasa, na pia vyama vya siasa vijiongeze kwa suala hilo.

Kuwe na mijadala ya jinsi ya kukuza uchumi kwa mbinu tofauti au nyinginezo, kwa mfano kupanua wigo wa uhuru wa uchumi, kwani watu wanaongezeka, ila rasilimali kama ardhi, maji na samaki haviongezeki.

# 13,000 wapata chanjo corona

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

UONGOZI wa Mkoa wa Rukwa umefanikiwa kutoa chanjo ya UVIKO-19 kwa wananchi wapatao 13,189, tangu ulipopokea chanjo hizo.

Mkuu wa mkoa huo, Joseph Mkirikiti, aliyasema hayo juzi, wakati akifungua kikao cha kamati ya ushauri ya mkoa huo, kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano uliopo katika jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Alisema Idara ya afya imefanikiwa kutoa chanjo hizo, ambapo ni sawa na asilimia 73.3, hivyo bado wananchi wanatakiwa kujitokea kupata chanjo hiyo kwa kuwa bado zipo.

Mkirikiti alisema kuwa suala la kupata chanjo ni muhimu na ni hiyari ya mwananchi, lakini ni muhimu kwa kuwa asiyepata chanjo hiyo, anaingia gharama kubwa za matibabu pale anapougua.

Aliwataka wananchi kujitokeza kupata chanjo hiyo kwa kuwa ni muhimu kwa usalama wa familia zao.

**Mkuu wa mkoa huo, Joseph Mkirikiti, aliyasema hayo juzi, wakati akifungua kikao cha kamati ya ushauri ya mkoa huo, kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano uliopo katika jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.**

# Wazazi wakumbushwa kusimamia maadili ya watoto

**Na Julieth Mkireri,**
CHALINZE

WAZAZI wamekumbushwa kusimamia maadili ya watoto wanaohitimu kidato cha nne mara baada ya kuondoka shuleni badala ya kuwaacha tu na hatimaye kujiingiza, kwenye makundi yanayochangia mambo maovu.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete, katika mahafali ya nane ya Shule ya Sekondari Mdaula, Halmashauri ya Chalinze.

Ridhiwani alisema wazazi hawatakiwi kuchoka katika malezi ya watoto, hasa baada ya kuhitimu elimu ya sekondari kwa kuwa vitendo vya baadhi yao kuiachia dunia, wako walimu wazuri na wabaya, ambao watawafundisha vibaya na kuharibu sifa ya shule.

"Wahitimu nendeni mkawape heshima wazazi wenu kwa kutangaza vyema Shule ya Mdaula. Maadili mliyofundishwa kutoka shuleni mwende mkayafuate hata baada ya kutoka hapa na wazazi msiwaache hawa watoto peke yao, mkaiachia dunia," alisema.

Pia aliwataka wazazi kusomesha watoto wao kwa bidii, ili wasaidie jamii katika maendeleo na kuondokana na hali ya umaskini, ambayo inachangiwa na kutojiendeleza kielimu. Alisema hatua hiyo husababisha uwapo wa idadi kubwa ya waajiriwa kutoka nje, kwenye kampuni zinazowekeza katika halmashauri hiyo.

Mbunge huyo aliahidi kupeleka kompyuta mpakato sita katika shule hiyo, kwa ajili ya somo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Kuhusu umaliziaji wa vyumba vya maabara, alisema tayari halmashauri imetenga Sh. million 30.

Mwenyekiti wa Bodi ya shule hiyo, Yusuph Khalfan, alisema shule hiyo ina uhitaji wa hosteli, kwa ajili ya kuwanusuru wanafunzi wa kike kutokana na kutoka maeneo ya mbali na shule.

Khalfan aliwataka wazazi kuwekeza kusomesha watoto, pia kuwa na mwamko katika uchangiaji wa mandeleo ya elimu badala ya kuacha kazi hiyo kwa serikali pekee.

Mkuu wa Shule hiyo, Melkizedeck Komba, alisema shule hiyo, ambayo ilianzishwa mwaka 2011 ikiwa na wanafunzi 78, kwa sasa ina wanafunzi 1,028 huku ikikabiliwa na uhaba wa vitabu, mabweni na walimu wa masomo ya sayansi.

Komba aliwashukuru wadau mbalimbali wanaosaidia kutatua kero za elimu, akiwamo Jackson Mushi, ambao wamekuwa wakiisaidia serikali kuondoa vikwazo katika shule hiyo na kuwaomba wengine kuendelea kujitokeza.




Wanufaika wa miradi kutoka Taasisi isiyo ya serikali ya Ladies Joint Forum (LJF) na baadhi ya viongozi kutoka kata ya Vingunguti jijini Dar es Salaam, wakimsikiliza Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Franscisca Mboya (hayupo pichani), wakati wa uzinduzi wa kampeni ya miezi mitatu yenye lengo la kuhamasisha wanawake na wasichana kupata chanjo ya UVIKO-19. **PICHA: ZUWENA SHAME**

# DED aahidi kufuatilia malipo ya walimu kituo cha wenye ulemavu

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Hassan Njama Hassan, amesema wanaendelea na utaratibu wa kufuatilia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) malipo ya uendeshaji wa shule ya elimu maalum Amani wilayani hapa.

Malipo hayo yalikwama tangu mwaka 2017 walipoingia mkataba wakati shule hiyo inaanzishwa.

Mkurugenzi huyo alisema hayo jana kuwa licha ya shule hiyo kufunguliwa, bado ina upungufu wa walimu wa kuwezesha kukidhi mahitaji kielimu kwa watoto wenye ulemavu.

Kwa sasa, alisema halmashauri hiyo ina vituo 21 vyenye mahitaji maalum wanavyovihudumia kupitia TAMISEMI katika huduma mbalimbali.

Awali, Mkurugenzi wa shule hiyo iliyomilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo la Morogoro, chini ya kituo cha kulea watoto wenye ulemavu na viungo na akili cha Amani, Padri Beatus Sewando, alisema walikubaliana na halmashauri kusaidiwa kwenye upatikanaji wa walimu, mishahara ya walimu, vitabu, ruzuku ya chakula na vifaa vingine vya elimu.

Padri Sewando alisema wanahitaji msaada huo kwa sababu uwezo wa wazazi na walezi wa watoto hao kumudu gharama hizo ni mdogo na ndiyo maana wamewekwa makubaliano hayo katika fomu iliyotiwa saini na pande zote mbili.

Alisema mpaka sasa shule hiyo ya msingi yenye madarasa manane, mabweni na ofisi za utawala ina walimu wanane, wanawake wakiwa watano na wanaume watatu ambao wanatoa elimu kwa wanafunzi 70 waliopo kwa kujitolea wakisaidiwa fedha kidogo za kujikimu na kanisa.

"Wakati tunaanzisha shule hii tulikubaliana na serikali kupitia halmashauri kimkataba na mikataba ipo. Tuliandikishiana kuwa wao walipe mishahara ya walimu na nesi na kuleta bajeti ya chakula kwa watoto pamoja na kushughulikia gharama zote za uongozi na sisi tushughulike na watendaji wasio na taaluma. Sasa wao hawajatekeleza majukumu yote tunayafanya sisi tena kwa shida sana," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alisema wanafunzi wanaosoma shuleni hapo hulazimika kukaa bweni na gharama za chakula za kutwa nzima zinahitajika, hivyo kwa hali ya kituo ilivyo kwa sasa ni ngumu kutimiza mahitaji yote ingawa jimbo linajitahidi kutekeleza.

Padri Sewando aliiomba TAMISEMI kutekeleza makubaliano waliyojiwekea kwenye mkataba na kutimiza mahitaji ya watoto ambao wametoka kwenye familia maskini ambazo hazina uwezo wa kuwasaidia kwa lolote.

"Walimu waliopo wanalipwa na jimbo posho ya Sh. 150,000 kwa mwezi ili wasife moyo na waendelee kujitolea kuwafundisha watoto," alisema.

Sewando alisema suala la halmashauri kutotoa ushirikiano kama walivyokubaliana, linachangia kwa kiasi kikubwa watoto kukosa chakula na huduma za matibabu kwa wakati kwa sababu kituo kwa sasa hakina wafadhili wa kukiendesha kama ilivyokuwa zamani.

# DC awatangazia vita machinga wanaokaidi kuhamia eneo rasmi

**Na Julieth Mkireri,**
KIBAHA

MKUU wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, ameamuru wafanyabiashara katika eneo la Picha ya Ndege kuhamia katika eneo Misufini ambalo limetengwa kwa ajili yao na Shirika la Elimu Kibaha.

Msafiri ametoa agizo hilo jana baada ya kutembelea Picha ya Ndege ambako wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga, wamekuwa wakifanya shughuli zao kwenye hifadhi ya barabara.

Alisema tayari ameshatoa agizo mara nne wafanyabiashara hao kuhamia katika eneo walilotengewa lakini hawajafanya hivyo, hivyo kusisitiza kuwa kuanzia jana, mfanyabiashara atakayekaidi agizo hilo atachukuliwa hatua za kisheria.

Pia aliwaagiza wafanyabiashara wenye maduka kuhakikisha wanafanya usafi kwenye maeneo yao na miundombinu iliyojengwa na serikali. "Wenye maduka fanyeni biashara kwa mujibu wa leseni zenu. Nikikuta unafanya biashara za sokoni hatua zitachukuliwa," alisema.

Ofisa Biashara wa Halmashau ya Mji wa Kibaha, Adolf Msangi, alisema tayari kuna wafanyabiashara leseni zao zilishapokonywa kwa kushindwa kufuata masharti na watafikishwa mahakamani kwa tuhuma zaidi za kisheria.

Mkuu wa Idara ya Mazingira wa Halmashauri hiyo, Mkana Mkana, alisema kwa sasa wanapendekeza adhabu ya faini kwa mfanyabiashara ambaye anakiuka kufanya usafi kwenye eneo lake iondoke na badala yake iwe ya kifungo cha miezi sita.

Mkana alisema usimamizi wa wafanyabiashara kutakiwa kuhama katika eneo hilo ulitarajiwa kuanza jana na kwamba hatua zitaanza kuchukuliwa kwa wanaokiuka na watakaokuwa hawazongatii usafi.

Katika hatua nyingine, baadhi ya wafanyabiashara walilalamika jana asubuhi kuwa wamevinjiwa na kuchomewa meza zao kwa madai ya kukaidi kuondoka katika eneo hilo na kuhamima Misufini.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Ester Kugwire, alisema usiku wa kuamkia jana, baadhi ya meza zilichomwa moto na bidhaa zingine hazijaonekana mpaka wakati huo.



Mkuu wa Kituo cha Polisi Bugarama, mkoani Shinyanga, Nestory John, akieleza jinsi wanavyoshirikiana na Kamati za Mpango kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), kupambana na ukatili huo, chini ya mradi wa "Kama", unaotekelezwa na mashirika ya Huheso Foundation na Rudi kwa ufadhili wa serikali ya Ubelgiji, wakati wa mafunzo yaliyofanyika katika kata ya Bugarama, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Samaki, dagaa kuwa mazao ya kimkakati

**Na Pendo Thomas,**
KIGOMA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imekusudia kupandisha hadhi dagaa na samaki wa Ziwa Tanganyika kuwa zao la kimkakati litakaloongezwa thamani na kuuzwa ndani na nje ya nchi hatua itakayochochea kukua kwa uchumi.

Hayo yalibainishwa juzi na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akiwa mkoani Kigoma katika ziara yake ya kikazi.

Ulega alisema utekelezaji wa mpango wa dagaa na samaki kuwa zao la kimkakati utaendana na utatuzi wa changamoto zinazoikabili sekta ya uvuvi.

"Hapa tuna mazao yetu ya kimkakati na tumeyadhamiria yapande hadhi na nyie tuungeni mkono. Tunataka yainue Kigoma, wavuvi wainuke pawe shime kabisa," alisema Ulega.

Aliema mpango huo utasaidia kuondoa tatizo la dagaa kuharibika hasa kipindi cha mvua ambacho hushindwa kukauka. Alisema mpango huo utaendana na uanzishwaji wa viwanda vya uchakataji utakaosaidia kupandisha thamani.

Paulo Samweli, Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika Mwalo wa Kibirizi, alisema wavuvi wameendelea kukumbana na vitendo vya ujambazi ndani ya Ziwa Tanganyika ambavyo vinapaswa serikali itoe utatuzi wa haraka ili kuwawezesha kuendelea kufanya shughuli zao kwa usalama.

Alisema matukio hayo yamekuwa yakitishia usalama wao pamoja na kuwarudisha nyuma kwa kuwa zana zao za uvuvi zimekuwa zikiporwa na majambazi, hivyo baadhi yao kusitisha shughuli hizo.

Pia aliiomba serikali kuwapatia mikopo yenye riba nafuu au isiyo na riba itakayowasaidia kununua zana bora za uvuvi ambazo zitaongeza uzalishaji.

Naye diwani wa Bangwe manispaa ya Kigoma Ujiji, Hamis Betese, aliomba uharakishwaji wa ujenzi wa mwalo wa Katonga ili wafanyabiashara wawe na sehemu nzuri ya kununua na kuuzia mazao ya uvuvi hatua itakayoongeza mapato ya serikali kupitia uvuvi.

# Usambazaji vifaa tiba wafikia 90%

**Na Abdallah Khamis** MTWARA

BOHARI Kuu ya Dawa (MSD) Kanda ya Mtwara imetekeleza agizo la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa la kusambaza dawa, vifaa tIba na vitendanishi vya maabara kwa zaidi ya asilimia 90.

Kaimu Meneja wa MSD Kanda ya Mtwara, Tea Malay, alisema hayo jana juu ya utekelezaji wa agizo hilo lililotolewa Oktoba 10, mwaka huu na Waziri Mkuu kutaka vifaa hivyo vifikishwe katika vituo vya kutolea huduma za afya ndani ya siku saba.

Alisema baada ya agizo hilo, MSD kupitia Mkurugenzi Mkuu wake, Meja Jenerali Gabriel Mhidze, iliweka mikakati kuhakikisha kila kanda inatekeleza jukumu hilo ndani ya muda kwa ajili ya kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi kwa wakati na bila usumbufu.

Malay alisema MSD Kanda ya Mtwara inahudumia mikoa ya Mtwara, Lindi na wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma.

"Sisi Kanda ya Mtwara baada ya agizo la Waziri Mkuu, tulijipanga kwa kuweka mikakati mbalimbali tukaangalia ni nini kinahitajika katika kutekeleza lakini tukawa na moyo kwamba lazima tutaweza. Tukaagiza dawa za kutosha kutoka makao makuu, tukaongeza muda wa kazi na vijana wa kufanya kazi ili tuendane na muda," alisema Malay

Meneja huyo alisema taratibu zote za kushusha na kupakia kwa umakini dawa hizo kazi ilifanyika kwa uhakika mkubwa na kufika katika maeneo yaliyokusudiwa kwa wakati.

Aliwashukuru waganga wakuu wa wilaya na mikoa kwa kukubali kutumia muda wa ziada kuhakikisha dawa na vifaa tiba vinapokewa katika maeneo yao.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Dk. Salvio Wikesi, alisema tangu Waziri Mkuu alipotoa agizo hilo, wamepambana na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa ikiwa ni pamoja na wilaya yake kusambaziwa vifaa tiba kwa asilimia 60.

Naye Dk. Dismas Masuluhu, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mtama, alisema changamoto alizoshuhudia Waziri Mkuu katika halmashauri yake za kutaka zitatuliwe, zimeshafanyiwa kazi kwa asilimia 80 na sasa kila kitu kinakwenda sawa.

**Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Dk. Salvio Wikesi, alisema tangu Waziri Mkuu alipotoa agizo hilo, wamepambana na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa ikiwa ni pamoja na wilaya yake kusambaziwa vifaa tiba kwa asilimia 60.**

## Vingunguti kuhamasishwa chanjo Uviko-19

**Na Zuwena Shame**

TAASISI isiyo ya serikali ya Ladies Joint Forum (LJF) imezindua kampeni ya miezi mitatu yenye lengo la kuhamasisha wanawake, wasichana na wakazi waishio kata ya Vingunguti na maeneo ya jirani mkoani Dar es Salaam kuchanja chanjo ya kujikinga na UVIKO-19.

Akizungumza na Nipashe baada ya uzinduzi huo, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, Fransinca Mboya, alisema chanjo ya UVIKO-19 kwa wakazi wa Kata ya Vingunguti imekuwa ya kusuasua na hali hiyo imetokana na imani potofu na taarifa zisizo sahihi.

Mboya alisema Vingunguti ni kubwa na ina watu wengi ikilinganishwa na kata zingine jijini Dar es Salaam, pia ina machinjio na minada mbalimbali, hivyo watu wake wako katika hatari ya kupata magonjwa mbalimbali kikiwamo kipindupindu na UVIKO-19 iwapo hatua za kujikinga hazitachukuliwa mapema.

"Tumeona athari za magonjwa mbalimbali ya mlipuko katika kata hii, hivyo ni vyema kutoa elimu na miongozo sahihi juu ya kuchanja kama kinga dhidi ya UVIKO-19 ili wakazi wa kata hii waishi na amani na kuendesha shuhuli zao za maendeleo za kila siku," alisema Mboya.

Mboya alisema kuwa pia ufuatiliaji wa ushauri wa kitaalamu dhidi ya chanjo ya UVIKO-19 ni mdogo sana kwa Kata ya Vingunguti, hivyo ni muda mwafaka kata hiyo kupewa elimu na miongozo sahihi kutoka serikalini na Shirika la Afya Duniani (WHO) ili watu wake waweze kuchanja.

Akizungumzia kampeni hiyo ya UVIKO-19 ambayo iliambatana na semina ya kuwajengea uwezo mabalozi kutoka mitaa yote ya Vingunguti, Mboya alisema walengwa hasa ni wanawake na wasichana kuanzia miaka 18 na 35, wenye ulemavu mbalimbali na hata wazee kwani ni wengi na wanaishi katika maisha hatarishi ikilinganishwa na wanaume.

Aliongeza kampeni hiyo inatarajia kuwafikia wanawake na wasichana moja kwa moja wapatao 200 na idadi zaidi ya 2000 isiyo moja kwa moja katika kata zote za Vingunguti na jirani.

# Kichwa kikubwa, mgongo wazi sasa tishio kwa ndoa

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Wazazi Wenye Watoto wa Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi Tanzania (ASBAHT), kimesema, asilimia 70 ya ndoa za wanachama wake zimesambaratika kutokana na uelewa mdogo kuhusu ulemavu huo.

Mratibu wa chama hicho Hidaya Alawi ndiye aliyesema hayo jijini Dar es Salaam juzi katika kikao cha ASBAHT, kilichokuwa kikijadili maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Watoto Wenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi. Maadhimisho hayo yanatarajiwa kufanyika Oktoba 25, mwaka huu jijini Dar es Salaam yakishirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wazazi wenye watoto walio na ulemavu huo, madaktari na viongozi wa serikali.

"Chama chetu kina wanachama 2,545, lakini asilimia 70 ya ndoa za wanachama wetu zimesambaratika baada ya wanaume kukimbia wake zao au kuwafukuza kwa kuzaa watoto wenye ulemavu huo," alisema Hidaya.

Hidaya alisema, yeye ni miongoni mwa watu ambao walikimbiwa, na kwamba sababu kubwa ni uelewa mdogo wa baadhi ya wanaume kuhusu watoto kuzaliwa wakiwa na ulemavu huo.

"ASBAHT ina matawi katika mikoa 10 ya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Mbeya, Mwanza, Mara, Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga, tumekuwa tukipokea kesi za aina tofauti kutoka huko," alisema.

Alisema, inawezekana tatizo ni kubwa zaidi katika maeneo ambayo hawajafikwa, ambapo wana mkakati wa kufungua matawi nchi nzima, na kwamba kesi wanazopata kwa sasa ni za wanachama tu.

Daktari bingwa wa mishipa ya fahamu na ubongo Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar, Dk. Seif Lali, alisema, kubadili mfumo wa ulaji wa vyakula kwa kuacha mazoea, ni njia mojawapo ya kumaliza tatizo hilo.

Wanaume waache kukimbia wake zao, bali wazingatia lishe bora hasa vyakula vyenye wingi wa madini ya foliki asidi kama mboga za majani kuanzia mchicha, spinachi, kabichi na vingine," alisema Dk. Lali.

Mbali na vyakula hivyo, anataja matunda kama maembe, maparachichi, mapapai na ndizi, lakini na nafaka kama mahindi, mihogo na mazao jamii ya kunde, pia mayai, samaki, nyama na maini.

"Vyakula hivyo vianze kuliwa miezi miwili na nusu au mitatu kabla ya kubeba ujauzito na pia ipo haja ya kuwawahisha watoto hospitalini pale wazazi wanapoona dalili za ulemavu huo na siyo kukimbiana.

Daktari bingwa wa watoto kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Hydom, Dk. Joshua Gideon, alisema, mtoto anaweza kuzaliwa akiwa hana ulemavu wa kichwa kikubwa, lakini baadaye akaupata.

"Kwa mfano akipata ugonjwa wa uti wa mgongo au kupata ajali ama jeraha kichwani halafu damu ikavujia kwenye ubongo, anaweza kupata ulemavu huo, hivyo wazazi wote wanapaswa kulijua hilo," alisema Dk. Gideon.

Aidha, alifafanua kuwa ulemavu wa mgongo wazi mtoto anaupata tangu tumboni, kwamba hawezi kuupata baada ya kuzaliwa, anbapo amesisitiza wazazi wote kuzingatia lishe inayotakiwa.



Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania anayemaliza muda wake, Hisham Hendi (kulia), akizungumza na Balozi wa Uingereza hapa nchini, David Concar (katikati) wakati wa hafla ya kumuaga Hendi, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji mpya wa Vodacom, Sitholizwe Mdlalose. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rukwa yatangaza donge nono kijiji utunzaji mazingira

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

SERIKALI mkoani Rukwa imetangaza zawadi nono kwa kijiji kitakachofanya vizuri utunzaji mazingira na Msitu wa Hifadhi ya Mbizi ambao ni mojawapo ya vyanzo vya maji kwa wakazi wa Manispaa ya Sumbawanga.

Akizungumza jana na viongozi wa Hifadhi ya Msitu wa Mbizi alipokuwa katika ziara ya kukagua maendeleo ya msitu huo, Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, alisema msitu huo ni muhimu kutunzwa licha ya kuwa ni chanzo cha maji, pia kuna miti adimu pamoja na wanyama mbalimbali wakiwamo mbega wekundu.

Aliwaagiza watendaji wa serikali kuhakikisha msitu huo unakua salama ili vitendo vya uchomaji moto viishe pamoja na shughuli nyingine za kibinadamu zisiwapo katika msitu huo.

Pia, aliwaonya wananchi wanaoishi vijiji vinavyozunguka eneo la hifadhi ya msitu wa Mbizi kuacha kuchungia mifugo yao ndani au karibu na mazingira ya msitu huo kwa kuwa wanyama hao wamekuwa ni chanzo kikubwa cha uharibifu wa msitu huo.

Awali, akitoa taarifa kwa mkuu wa mkoa huo, Mhifadhi mkuu wa msitu wa Mbizi, Mohamed Kyangi, alimwambia kuwa changamoto kubwa wanayokabiliana nayo katika utendaji kazi ni baadhi ya wananchi kuchoma moto msitu huo.

Alisema hifadhi hiyo imekuwa ikitumia fedha nyingi kwa ajili ya kuzima moto unapotokea, fedha ambazo zingetumika katika kuotesha miti kwenye vitalu na kuwagawia wananchi ambao nao wangepanda kwenye mazingira yao ili kukabiliana na majanga ya asili yanayowapata kutokana na kukata miti ovyo.

# Corona yadhihirisha lishe duni

**Na Mary Geofrey**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Dk. Germana Leyna, amesema maambukizi ya UVIKO-19 yameakisi hali ya lishe kwa Watanzania siyo nzuri kutokana na namna ambavyo yamewaathiri watu wengi na wengine kupoteza maisha.

Alisema lishe bora husaidia kuimarisha kinga ya mwili na husaidia kupunguza ukali wa maradhi pamoja na vifo vitokanavyo na magonjwa ya kuambukiza ikiwamo UVIKO-19.

Dk. Leyna alieleza hayo juzi jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Lishe Kitaifa, yatakayofanyika mkoani Tabora kuanzia Oktoba 18 hadi 23 mwaka huu.

Aliwataka wananchi kuzingatia mlo kamili kutoka katika makundi matano ya chakula ili kuepuka maradhi mbalimbali yasiyo ya kuambukiza na kuambukiza ikiwamo utapiamlo na kiribatumbo.

"Hivyo Siku ya Lishe Kitaifa ni jukwaa muhimu katika kutekeleza na kuendeleza azma ya serikali kutokomeza aina zote za utapiamlo nchini na kuendeleza jitihada za serikali," alisema Dk. Leyna.

Alisema pia maonyeshe hayo yatachangia katika kuongeza uelewa na ufahamu juu ya lishe bora na hatua chanya hususani katika ngazi ya kaya na jamii.

Alisisitiza kuwa pia wanaendelea kutoa dawa za kutibu wagonjwa wenye utapiamlo mkali na kadiri, kuanzisha siku maalum ya kuadhimisha mafanikio ya jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na kuendelea kuhamasisha umma kwa kutoa elimu kuhusu faida za lishe bora na athari zake katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Alisema katika maadhimisho hayo wanawaleta pamoja wadau wa lishe ambao ni viongozi, wanasiasa, watendaji, wataalamu, wadau wa maendeleo, mashirika yasiyo ya kiserikali na wananchi ili kuongeza ufahamu kuhusu umuhimu wa lishe kama ni msingi wa afya bora na maendeleo ya kiuchumi na jamii.

"Kwa mwaka huu kilele chake kitakuwa Oktoba 23 katika viwanja vya Nanenane mkoani Tabora na kauli mbiu inasema 'Lishe Bora ni Kinga Thabiti dhidi ya Magonjwa; Kula Mlo Kamili, Fanya Mazoezi, Kazi Iendeleee," alisema Dk. Leyna.

Alisema katika maonyesho hayo watatoa elimu kwa jamii, namna ya kutayarisha mlo kamili kutoka makundi matano ya chakula, kuelekeza kwa vitendo namna ya kupika mlo kamili ili kusaidia kuwajengea wananchi uelewa.




Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, akikata utepe kuzindua rasmi kongamano la tatu la wanawake na biashara lililoandaliwa na Benki ya Biashara Tanzania (TCB), jijini Mwanza juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mti ulioshindikana kukatwa kwa greda

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MTI wa ajabu wa asili ambao ulikuwa ukitumiwa kufanya matambiko na jamii kwa ajili ya utatuzi wa masuala mbalimbali uliopo katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, umekuwa kivutio kwa wageni wanaotembelea hifadhi hiyo kutokana na kushindikana kukatwa wakati wa upanuzi wa barabara.

Mti huo unaofahamika kama marula, umekuwa kivutio kutokana na kuwa katikati, hivyo eneo hilo kuwekwa barabara pacha baada ya kushindwa kuondolewa wakati wa upanuzi ndani ya hifadhi hiyo ikitokea Kijiji cha Mloka wilayani Rufiji mkoani Pwani.

Ofisa Uhifadhi Mwandamizi, Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, Seth Mihayo, alisema umekuwa kivutio kwa sababu wakati wa upanuzi huo wa barabara licha ya kutumia vifaa vya kisasa kama magreda ya kukata miti mikubwa, mti huo ulishindikana kukatika na kuwa vifaa hivyo licha ya kuwa vya kisasa, lakini viliishia kuharibika na mti huo kuendelea kubaki.

Alisema hata pale walipojaribu kuleta mitambo mingine yenye uwezo zaidi, pia ilishindikana kuuondoa, hivyo kuharibika na kuachwa katika eneo hilo, huku barabara hiyo ikitengenezwa kuwa pacha.

Alisema baada ya kufanyika kwa utafiti historia inaonyesha kulikuwa na vijiji kipindi cha nyuma ndani ya hifadhi hiyo kikiwamo Mloka na kuwa mababu na wazee wa miaka ya nyuma walikuwa wakifanya mambo ya mizimu na matambiko mbalimbali hivyo wameamua kuenzi kwa kuacha mti huo ili uwe sehemu ya kivutio cha utalii.

**Mti huo unaofahamika kama marula, umekuwa kivutio kutokana na kuwa katikati, hivyo eneo hilo kuwekwa barabara pacha baada ya kushindwa kuondolewa wakati upanuzi ndani ya hifadhi hiyo ikitokea Kijiji cha Mloka wilayani Rufiji mkoani Pwani.**

# DC awahimiza wananchi kulipa kodi kwa wakati

**Na Mwandishi Wetu,** MBINGA

MKUU wa Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma amewahimiza wafanyabiashara na wananchi kulipa kodi kwa wakati kwa kuwa kodi hiyo hurudi kwao kupitia miundombinu na miradi mbalimbali ya maendeleo.

Aziza Mangosongo alitoa rai hiyo jana alipozungumza na timu ya maofisa kutoka Mamlaka ya Mapato (TRA) Makao Makuu Dar es Salaam walipowasili wilayani humo kwa ajili ya kufanya kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango.

Mkuu wa wilaya huyo alisema kodi hulipwa na watu wote wakiwamo watumishi wa serikali na wa sekta binafsi, wakulima, wafugaji, wavuvi pamoja na wafanyabiashara. Alisema tofauti iliyopo ni kwamba, kodi inayolipwa na watumishi hukatwa moja kwa moja kupitia mishahara yao.

"Ninapenda kuchukua fursa hii kuwahamasisha na kuwakumbusha wafanyabiashara na wananchi wote kulipa kodi kwa wakati ili kuinua uchumi wa nchi yetu na tuondoe ile kasumba ya kusema kwamba watumishi wa serikali hawalipi kodi, watumishi tunakatwa kodi moja kwa moja kupitia mishahara yetu," alisema.

Kiongozi huyo wa serikali aliwataka wananchi kuwafichua watu wanaokwepa kulipa kodi kwa kutoa taarifa sahihi za wahusika hao katika maeneo mbalimbali ili washughulikiwe.

"Pia, ninawaomba tusisite kuwataja watu wote wanaokwepa kulipa kodi na tujitahidi kutoa taarifa sahihi za wakwepa kodi katika maeneo yetu kwa maana kodi ni afya na ni uhai wetu," alisema.

Meneja wa Huduma kwa Mlipakodi kutoka TRA Makao Makuu, Honester Ndunguru, akiitambulisha timu ya maofisa wanaofanya kampeni hiyo, alisema TRA imejipanga kufikia idadi kubwa ya wafanyabiashara nchini kwa ajili ya kuwaelimisha kuhusu haki na wajibu wao katika suala zima la ulipaji kodi.

"Sisi kama TRA, tumejipanga kufika maeneo mbalimbali kuhakikisha tunawaelimisha walipakodi wetu kujua haki na wajibu wao na leo tumekuja hapa Mbinga kwa lengo hilo hilo la kuhakikisha tunawafikishia elimu ya kodi wafanyabiashara wa wilaya hii," alisema.

Timu ya maofisa wanaofanya kampeni ya elimu kwa mlipakodi mkoani Ruvuma iko wilayani Mbinga ikiendelea kutoa elimu ya kodi na baada ya wilaya hiyo, itaelekea Wilaya za Nyasa, Namtumbo na Tunduru.

WAZIRI DK. MWIGULU:
Ustadi wake Rais Samia umeleta mkopo nafuu trilioni 1.3/- za IMF
Ukurasa 12





Ukurasa 13
Muongo mmoja wa kazi shirika lilivyowafikishia haki milioni 6.4



# Mkutano vyama, polisi, msajili fupa linaloelekea kuvunja meno

**Na Sabato Kasika**

IKIWA imebakia siku moja kabla ya kufanyika mkutano baina Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Jeshi la Polisi na vyama vya siasa, hatima ya kikao hicho inaendelea kubaki kuwa sintofahamu.

Kinachodaiwa kuwa ni mkwamo kinatokana na vyama vikuu CHADEMA, NCCR-Mageuzi kukataa kushiriki , wakati mmojawao akimpa masharti Msajili, huku ACT-Wazalendo kikibaki kimya bila kueleza iwapo kitahudhuria au lah.

Mkutano huo unaopangwa kufanyika kesho jijini Dodoma, umepokelewa na masharti kutoka CHADEMA ikiitaka Ofisi ya Msajili iruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa na pia Mwenyekiti Freeman Mbowe, aachiwe bila masharti.

"Kamati kuu imeshakubaliana kutoshiriki mkutano huo, hadi kwanza Msajili aruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa na pia tunataka mwenyekiti wetu, Mbowe, aachiwe bila masharti ili aongoze chama kwenye mkutano huo," anasema Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itifaki na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema.

Anataja sharti jingine kuwa ni kutaka wanachama wao walioko magerezani wakiwamo wafungwa na mahabusu kwenye maeneo mbalimbali nchini waachiwe huru.

"Bila msajili kufanyia kazi hayo masharti, hatuwezi kuhudhuria mkutano huo huku tukiwa wafungwa wa kisiasa. Tunataka tuwe huru kwanza kutoka kwenye kifungo hiki cha kuzuia mikutano ya hadhara," anasema.

### NCCR MAGEUZI HAIMO

Chama cha NCCR- Mageuzi kimetangaza kujiweka pembeni kwa madai kuwa hakikushirikishwa katika maandalizi lakini kukosekana uwazi.



Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, mwenyeji wa mkutano huo. **PICHA: MTANDAO.**

Aidha, kimedai watuhumiwa hawawezi kujipa kazi ya unyapara na usuluhishi, na kwamba hakuna mahali Msajili ameweza kutekeleza wajibu wake wa kisheria na kuongeza: " Msajili ni mtuhumiwa katika hilo, hawawezi kujipa kazi ya unyapara na usuluhishi....," anakaririwa na James Mbatia akizungumza na vyombo vya habari.

Mbatia Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi anadai mkutano na Msajili, hauna nia njema bali kufifisha na kubeza hoja zao halali za kuhakikisha taifa linakuwa na mfumo imara wa demokrasia.

"Ofisi ya Msajili wa Siasa na Jeshi la Polisi ambao ndiyo watuhumiwa wakubwa walikutana na kutoa msimamo wa kupotosha umma kwamba eti kuna upungufu wa sheria? Kazi ya polisi ni kusimamia sheria zilizopo," anasema.

Wakati NCCR-Mageuzi na CHADEMA, zikiweka msimamo wa kutohudhuria, Katibu Mkuu wa ACT- Wazalendo, Addo Shaibu, anasema chama chao kinaendelea kujadili iwapo kinashiriki au kukaa kando.

### WALIOKO TAYARI

Chama cha Alliance Democratic Change (ADC) ni miongoni mwa vyama vilivyokubali kushiriki katika mkutano huo, huku Katibu Mkuu , Doyo Hassan Doyo akisema meza ya mazungumzo ndiyo huleta mwafaka.

"Sisi ADC tutahudhuria mkutano na tayari tunayo barua ya mwaliko, tunaamini kuwa mkutano huo ni sehemu sahihi ya kufikisha kero ambazo tunaona zinahitaji kufanyiwa kazi na Msajili," anasema Doyo.

Katibu huyo anasema, mwaliko waliopewa wa kuhudhuria mkutano huo ni heshima kubwa kwao, hivyo wanaamini kuwa watakuwa na nafasi ya kumweleza Msajili yale yote ambayo yanaumiza chama chao.

"Ajenda zetu tulizopanga kuzifikisha kwa msajili siyo za kuandikwa magazetini, bali mtazisikia baada ya kumaliza mkutano huo ambao sisi tunauchukulia kwa uzito mkubwa," anasema.

### CUF NAO NDANI

Chama cha Wananchi (CUF), kinasema kitahudhuria mkutano huo kikiwa na ajenda tatu muhimu ambazo kinataka Msajili wa Vyama vya Siasa azipatie ufumbuzi ili siasa za Tanzania ziendelee kustawi.

Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Magdalena Sakaya, anataja ajenda hizo kuwa ni kutaka ufafanuzi wa kina kuhusu vyama vya siasa kuzuiwa kufanya mikutano ya hadhara kwa zaidi ya miaka mitano.

"Ajenda ya pili tunataka atuambie kwa nini polisi wanavamia vikao vya ndani vya vyama na kuvizuia na ya tatu tunataka atuambie kwa nini viongozi wa vyama vya upinzani wanakamatwa na kuwekwa kuzuizini," anasema Sakaya.

Anasema ndizo ajenda zao kuu ambazo wameona wahudhurie mkutano huo ili wapate majibu yake, kwa kuwa Msajili ndiye mlezi wa vyama vyote vya siasa anasimamia na kutekeleza sheria za vyama hivyo.

"Lakini pia anatakiwa kuhakikisha vyama vinakua na kushamiri, hivyo hayo ndiyo mambo ya msingi ambayo tunataraji yatolewe ufafanuzi wa kina na Msajili kwenye mkutano huo," anasema.

### MSAJILI AWATAKA MKUTANONI

Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, anatoa ufafanuzi akisema mwaliko huo una mambo mawili kuukubali au kuukataa na kwamba hawezi kutoa ufafanuzi wa vyama kutoa masharti ya kutekelezwa kwanza kabla ya mkutano, akieleza kuwa ni mambo ya kusikia kwenye vyombo vya habari.

"Ingekuwa busara kama wanaosema wametoa masharti, wakaja kwenye mkutano ili tujadili kwa pamoja kwani wote tuna lengo la kumaliza sintofahamu," anasema Jaji Mutungi.

Anafafanua kuwa mkutano huo una lengo la kuweka mazingira rafiki na maelewano baina ya vyama siasa, na kwamba wadau ni muhimu ili kufanikisha azma hiyo na kuhakikisha kila mmoja anashiriki na si kujiweka pembeni.

Anaeleza kuwa haoni kuwa ni busara vyama kuweka masharti kwenye jambo ambalo linalenga kumaliza kasoro zinazolalamikiwa na kwamba ni vyema badala ya kukataa mwaliko viukubali.

MIEZI SITA YA RAIS SAMIA



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba. **PICHA: MAKTABA**

WAZIRI WA FEDHA DK. MWIGULU:

# Ustadi wake Rais Samia umeleta mkopo nafuu trilioni 1.3/- za IMF

- Zitto aliloanzisha miezi minne, limekuwa
- Vita ya Uviko-19 yapatiwa silaha sahihi
- Salamu maalum za vita mazingira hatarishi

**Na Mwandishi Wetu**

TANGU kuingia kwake madarakani sasa yatimu miezi sita, mengi yanashuhudiwa katika harakati za Rais Samia Suluhu Hassan, kusukuma mbele maendeleo ya nchi.

Ni hatua za ndani na nje ya nchi, Rais akibeba nahau zote harakati zake za maendeleo ya kiuchumi kwa Watanzania, pia mazingira wezeshi nyumbani au kimataifa, sura ya matunda iko bayana, kwani kila siku kunazinduliwa mradi endelevu na wakati huohuo, mazingira bora yanatambuliwa.

Hivi karibuni, Rais Samia akiwa mwalikwa aliyefanya uwasilisho katika kikao cha Umoja wa Mataifa hivi karibuni na kuhutubia baraza hilo. Ni heshima kubwa kwa nchi kimataifa na hata ukanda wa Afrika Mashariki.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, anapozungumza katika uzinduzi wa Kampeni ya Maendeleo wa Ustawi wa Taifa na Mapambano ya UVIKO 19, anaainisha namna mazungumzo kati ya Rais Samia na Mkurugenzi Mtendaji wa IMF, Kristalina Georgieva, yalivyokuwa na mafanikio makubwa.

"Utakumbuka (Rais) ulifanya mkutano kwa njia ya mtandao na Mkurugenzi Mtendaji wa IMF, Bi. Kristalina Georgieva tarehe tatu Mei 2021. Pia Juni 29, 2021, ulifanya mkutano na Mkurugenzi wa IMF Kanda ya Afrika, Abebe Selassie," anatamka Dk. Mwigulu.

Anaainisha uwasilisho wa dhamira ya serikali nchini kutafuta mkakati wa muda mrefu kukabiliana na maradhi UVIKO 19 na athari zake kwa afya na uchumi wa umma.

Dk.Mwigulu anakumbusha hatua za kwanza kutekeleza azma ya maudhui ya mtandao huo, Rais Samia anaelekeza Wizara ya Fedha na Mipango kuratibu majadiliano katika ngazi ya wataalamu, kwa kushirikiana na sekta zote zilizoathirika, ikiwamo timu za wataalamu wahusika wa maradhi UVIKO-19.

**HATIMAYE MKOPO**

Ni mchakato wa mazungumzo kati ya serikali na IMF uliochukua miezi minne, kwani ilipotimu tarehe saba ya mwezi uliopita, Bodi ya Wakurugenzi ya IMF iliridhia kutolewa mkopo nafuu kwa serikali ya Tanzania (SMT), Dola za Marekani milioni 567.25, ambazo ni sawa na Sh. trilioni 1.3, mahsusi zikielekezwa kukabiliana na athari za UVIKO-19.

"Fedha hizo zinajumuisha mkopo nafuu usio na riba kupitia dirisha la 'Rapid Credit Facility' (RCF) wa jumla ya Dola za Marekani milioni 189.08," anasema Dk. Mwigulu, akifafanua ni sawa na theluthi moja ya mkopo wote.

Pia anataja kuwapo mkopo nafuu wenye riba ndogo (asilimia 1.05) kupitia dirisha liitwalo 'Rapid Financing Instrument (RFI)' wa Dola za Marekani milioni 378.17, sawa na theluthi mbili ya mkopo wote. Fedha hizo zinatakiwa kutumika katika mwaka wa fedha uliopo, 2021/22

Anasema katika mkopo wa RCF usio na riba una kipindi cha neema wa kutolipa kwa miaka mitano na nusu na malipo hayo yanatakiwa kuanza mnamo Machi, 2027 hadi Septemba, 2031.

Pia kupitia mikopo yenye masharti nafuu, una kipindi cha neema cha miaka 10 na robo na utakapoanza kulipwa utachukua mwaka mmoja na miezi tisa, Desemba, 2024 mpaka Septemba 2026.

Waziri anataja masharti yake ni: Kuhakikisha fedha zinaelekezwa katika kukabiliana na UVIKO-19; kutumia mkopo ndani ya mwaka uliopo wa fedha; kuweka wazi mikataba na taarifa za kampuni zitakazoshinda zabuni, ikijumuisha majina ya wamiliki wake.

Mengine anataja ni kutangaza taarifa za maambukizi na vifo vitokanavyo na UVIKO-19; kutoa taarifa za utekelezaji matumizi ya fedha hizo kila robo mwaka; kuweka mfumo wa ufuatiaji matumizi ya fedha walizopewa.

Kwa mujibu wa waziri, pia wanaohusika wanatakiwa kukamilisha utoaji taarifa za ukaguzi wa matumizi ya fedha za mkopo na kuandaa nyongeza ya bajeti baada ya mapitio ya nusu mwaka ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2021/22.

**ENEO LA TAHADHARI**

Waziri anasema penye shule madarasani nako hali siyo nzuri, akitoa mfano wanakostahili kukaa watoto 50 wanapatikana 350, hivyo ni hatari zaidi iwapo anapotokea mmoja kaambukizwa maradhi inawaweka wote katika hatari zaidi.

"Hivi hatuwezi kuongeza madarasa kuweka walau social distance (umbali kati ya mtu)?" anahoji waziri na anaendelea:

"Hivi kati ya fedha au deni na kuokoa maisha ya watoto wa Watanzania, kipi kina thamani zaidi? Kwenye hili, umezingatia kuwa 'form one' (kidato cha kwanza) ni toleo la kwanza la elimu bila malipo, hivi wanakwenda kuongezeka mara mbili."

Waziri Dk. Mwigulu anaelekeza mfano katika Vyuo vya Elimu ya Ufundi (VETA), kwamba kuna misongamano kwa sababu majengo yake mengi hayajakamilika.

"Rais ukawakumbuka na ukawajali mpaka wasioona kwa kusema watu hawa wanatokea makwao na wanachangia vitabu ni rahisi kuambukizana. Hivyo kwa FDC wanachangia vifaa vya kujifunzia," anasema.

Waziri anasema, licha ya mwamko kuitikia ushauri wa wataalamu kunawa maji tiririka ni njia ya kujikinga na UVIKO 19, anataja kuwapo maeneo mengi yenye misongamano ya watu yasiyo na huduma ya maji, mfano hai katika zahanati, shule, stendi za mabasi na masoko.

"Rais ulielekeza kuziangalia na sekta kama Maliasili na Utalii iliyoathirika kwa kiwango kikubwa. Jambo hilo limezingatiwa sambamba na kutunisha mfuko wa TASAF na Mfuko wa Vijana na Wanawake na Wenye Ulemavu," anahitimisha Mwigulu.

# Muongo mmoja wa kazi shirika lilivyowafikishia haki milioni 6.4

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Shirika la Huduma za Sheria (LSF), linaposherehekea miaka 10 ya uwepo wake, lina mengi ya kujivunia na kubwa zaidi ni watu zaidi ya milioni 6.4 waliofikiwa na huduma zake kwenye eneo la kusaka na kupata haki.

Muongo mmoja wa kuanzishwa kwake limewanufaisha Watanzania hususan wanawake kwa kuwaongezea uelewa kuhusu masuala ya kisheria na kupata haki zao za kijamii na kiuchumi.

Ili kutimiza lengo kuu la LSF la haki kupatikana kwa wote shirika lilianzisha mpango maalumu ambao kila aliyekosa huduma za msaada wa kisheria kwa urahisi, anazipata na kuzifurahia.

Wanawake na wasichana wako katika hali mbaya zaidi kwenye kupata haki zao ikilinganishwa na wanaume, lakini katika kushughulikia hilo na kuleta usawa, LSF ilianzisha Mpango wa Upataji Haki ambao unawaweka wanawake na wasichana katika msingi imara wa kupata haki.

Ili kufikia malengo ya mpango huo wa haki kwa urahisi, LSF imewekeza kwa wasaidizi wa kisheria ambao wapo ndani ya jamii ili kuwawezesha wanawake na wasichana kupata huduma za msaada wa kisheria kwa bei nafuu na kwa urahisi zaidi.



Wananchi wakifurahia mafanikio ya kazi ya huduma za msaada wa kisheria . **PICHA: LSF.**

Ili kuhakikisha utekelezaji wa mpango huo unafanyika kwa usahihi, LSF kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, Chama cha Wanasheria ya Tanganyika (TLS) na Shule ya Sheria ya Tanzania iliratibu mafunzo ya kuwandaa wasaidizi wa sheria zaidi ya 4,500 watakaohudumia wananchi Bara na Zanzibar.

Katika kila wilaya, watu 25 ambao wenye vigezo na viwango, pamoja na wananchi wengine walioandaliwa na kufundishwa kwa madhumuni ya kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa hiari, wapo kazini.

Wahitimu wa mafunzo hayo, walitakiwa kujipanga na kuanzisha shirika lisilokuwa na kiserikali wala la kibiashara ambalo limesajiliwa kikamilifu litakalofanya kazi katika ngazi ya wilaya.

Pia LSF ilianzisha mashirika ya kiraia yanayotoa ushauri wa kitaalam (RMOs), ambayo kazi yake kuu ilikuwa kusimamia na kuongoza kazi ya wasaidizi wa kisheria katika kila wilaya.

Kupitia usimamizi huo wa RMOs, shirika liliimarisha uwezo wa wasaidizi wa kisheria kupitia mafunzo kazini katika vipengele mbalimbali ikiwamo usimamizi wa fedha, utekelezaji wa programu, ufuatiliaji na tathmini, uhamasishaji na mawasiliano kwa madhumuni ili kuboresha utoaji wa huduma.

Umakini zaidi uliwekwa kwenye kuimarisha taasisi kuhakikisha miundo na mifumo iko sambamba na mashirika yote 183 ya kisheria ambayo yamesajiliwa kikamilifu na kufuata sheria na kanuni za asasi siziso za kiserikali (NGOs).

Kupitia ujuzi wa kisheria walioupata, wasaidizi hao wameendelea kutoa huduma za msaada wa kisheria chini ya udhamini wa mashirika yaliyosajiliwa kutekeleza jukumu hilo kwa watu wengi ambao huduma za msaada wa kisheria hazikuwafikia.

Mashirika hayo ya RMOs yamefuatilia uhusiano wa wasaidizi wa kisheria na LSF katika miaka ya mwanzo tangu kuanzishwa kwake wakati wakitekeleza miradi ambayo ilichangia kwa ufanisi kutimiza malengo mapana ya LSF. Malengo hayo yanalenga kuwapo kwa mazingira upatikanaji wa haki kwa kila mtu bila ubaguzi.

Uhusiano huu wa awali ulikuwa muhimu katika awamu ya pili ya Mpango wa Upataji Haki ambao ulianza mwaka 2016 na kumalizika mwaka 2020.

Pamoja na mambo mengine LSF ilishuhudia njia nyingi za ubunifu zilizoundwa na RMOs na kutekelezwa kwa ushirikiano na mashirika ya kisheria ili kupanua utoaji wa huduma za msaada wa kisheria.

"Jukumu letu linamaanisha kwamba lazima tufanye bidii zaidi kufikia malengo tunayoweka kwa shirika letu na mashirika ya kisheria yaliyo chini ya uangalizi wetu. Katika mkoa mkubwa kama Shinyanga lazima kuzingatia viwango ambavyo LSF inatarajia kuvipata kutoka kwetu lakini pia tuna malengo yetu kama shirika ambayo tunahitaji kufanya kazi kwa bidii ili kutimiza.

"Sehemu ya Mpango wa Upataji Haki ni fursa muhimu ya kutumia uwezo wetu", anasema John Shija Meneja wa Programu katika Kituo cha Paralegal Shinyanga (PACESHI), RMO wa eneo hilo.

Jambo la kipekee zaidi la mpango huu ni kwamba huduma hizi muhimu zinapatikana bure na kwa zaidi ya miaka hii 10 wamefaidika wanawake, wanaume, wasichana na wavulana kwa sawa.

Kwa kuwa walengwa hawalipii huduma hizi za msaada wa kisheria, LSF imepanua mzunguko wake na kuruhusu Watanzania wengi haswa wale walio katika ngazi za chini za jamii zilizopo vijijini kuzipata huduma hizo kwa urahisi.

Takwimu za ripoti za 2016 hadi 2020 zinaonyesha kuwa asilimia 56 ya watu waliofikiwa na msaada wa kisheria walikuwa wanawake wakati asilimia 44 ni wanaume. Aidha, wakati wale waliofikiwa kupitia msaada wa kisheria asilimia 55 walikuwa wanawake na 45 wanaume. Takwimu hizo zinaonyesha kuwa mpango huo unalenga zaidi kufikia wanawake lakini pia wanaume hufaidika.

Siri Liwawa ambaye ni Msaidizi wa sheria na Paza Sauti Foundation (PASAFO) huko Rufiji, Pwani anasema, "Watu tunaowahudumia wale wa hali ya chini kabisa, ni wale ambao wamekosa fursa ya kufikiwa kwa urahisi na huduma hizo, hivyo tunawasaidia kupata haki zao bila kuwa na wasiwasi wowote kuhusu suala la upatikanaji wa pesa ili kupata huduma hizo za msaada wa kisheria.

"Tunafanya kazi katika jamii zetu kwa kujitolea licha ya changamoto nyingi tunafanya kila tuwezalo kuendelea kutoa huduma hizi muhimu".

Ukweli huu unamaanisha kuwa wasaidizi wa kisheria ni miongoni mwa Watanzania waliojitolea zaidi kwa kuzingatia hali wanazokutana nazo katika kazi zao za kila siku.

Hutembea umbali mrefu kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa walengwa walio katika mazingira magumu kwani jamii nyingine huona haki ya kupata huduma za kisheria ni hatari kwao ndiyo maana hujenga uhasama na hata kutoa vitisho kwa wasaidizi hawa wa kisheria.

Kama kaulimbiu ya LSF inavyosema , "Haki kila siku kwa changamoto za kila siku", inaendana na malengo ya kila mshauri wa sheria anapoamka na kuanza kutimiza majukumu yake.

Changamoto kama vile migogoro ya ardhi, mivutano ya urithi, unyanyasaji wa kijinsia, kutelekezwa kwa watoto, mimba za utotoni na ukeketaji wa wanawake ni sehemu kubwa ya kesi ambazo wasaidizi wa kisheria hushughulikia mara kwa mara.

Ripoti ya mwaka 2020 ya LSF inaonyesha kuwa zaidi ya watu milioni 6.4 walifikiwa kupitia elimu ya kisheria iliyotolewa na wasaidizi wa kisheria, wakati asilimia 68 ya kesi ambazo wasaidizi wa kisheria walihudhuria walisuluhishwa kwa mafanikio.

"Tunashughulikia kila aina ya masuala ambayo jamii zetu zinakabiliana nayo ni sawa kusema kwamba huduma za kisheria tunazotoa zinawawezesha hata wale ambao mwanzoni waliamini kuwa hawana tumaini.

"Sisi ni sehemu ya jamii zetu na tuna jukumu la kuhakikisha haki inafurahiwa na kila mtu. Ni muhimu kusema kwamba utafiti tulionao na tunaotumia kila siku ni matokeo ya uboreshaji wa uwezo wa kawaida tunayopokea kutoka kwa shirika letu la washauri ambalo linajumuisha utekelezaji wa mradi, kuripoti, ufuatiliaji wa miradi na matokeo pamoja na usimamizi wa fedha ", anaelezea Japhet Lazaro wa Kibondo Paralegal Foundation (KIPAFO) huko Kigoma.

Ili kusaidia na kuwezesha ufikiaji wa huduma za msaada wa kisheria, wasaidizi wa kisheria pia hutumia njia zilizopo za kuungana na watu katika wilaya zao na hii ni pamoja na mikutano ya hadhara, vikao vya shule na wanafunzi, hafla za umma kama bonanza, ziara za vituo vya afya ambapo idadi kubwa ya wanawake wanaweza kufikiwa ikiwa ni pamoja na vipindi vya redio vinavyoonyesha uelewa wa jumla wa sheria na vipindi vya maswali na majibu.

Programu ya Haki Yangu inayopatikana kwenye simu janja (smart phone), ilizinduliwa mwaka jana na imekuwa jukwaa la msaada wa kisheria kwa yeyote mahali popote anapoweza kupata wasaidizi wa kisheria na kufaidika na elimu ya sheria au msaada wa kisheria.

Ni ukweli kwamba wakati mwingine wasaidizi wa kisheria hawawezi kutekeleza kazi za kisheria kama wanasheria au mawakili lakini RMOs kwa upande mwingine wanaweza kuwa na mawakili katika ofisi zao.

Jambo hili limekuwa muhimu katika kuhakikisha kesi ambazo zinahitaji utatuzi wa kisheria zaidi ya wigo wa wasaidizi wa sheria zinarejeshwa kwa ofisi ya RMO.

# Bibi Titi akumbukwa kwa tukio la kumuenzi kitaifa

**Na Gwamaka Alipipi**

NI wiki iliyopita Watanzania walimkumbuka Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, aliyewaacha ukiwa miaka 22 iliyopita, kikubwa kinachowagusa ni kuliunda Taifa la Tanganyika na baadaye Tanzania, kufuatia Muungano wake na Zanzibar mwaka 1964.

Kama inavyoelezwa kwenye harakati na mafanikio ya kufikia uhuru wa Tanganyika, nyenzo muhimu zinazofanikisha ushindi huo wa Mwalimu Nyerere , linajitokeza jina la Bibi Titi Mohamed maarufu Mama Shujaa wa Tanzania.

Tofauti ya tarehe zao za vifo, zinapishana, kwa wastani wa wiki tatu, wakati Nyerere alifariki Oktoba 14, 1999, Bibi Titi alifariki Novemba 5, 2000 ikiwa ni mwaka mmoja baada ya Mwalimu.

Baba wa Taifa, akiwa ameshika usukani wa kukiongoza chama cha TANU, moja ya njia alizotumia kuufikia umma ni makundi ya kijamii yakiwamo vijana, wafanyakazi, wazee na wanawake, kundi ambalo mzizi na msingi wake anapatikana Bibi Titi.

Mara baada ya kukabidhiwa uongozi wa TANU Nyerere katika harakati zake za kuwafikia kinamama , alijipenyeza Kariakoo Dar es Salaam, ambako si mbali sana na uliko ukumbi wa DDC, alipogonga hodi na kuwafikia kikundi cha wanawake wajasiriamali, akiwataka wamuunge mkono kumng'oa mkoloni.

Mahsusi jicho lake likiwa limemfikia aliye miongoni mwao `shapu' alipatikana Bibi Titi Mohamed, ambaye ameacha rekodi kwa namna alivyochangamkia jukumu hilo, binafsi na katika 'staili ' ya kuwaunganisha kinamama kitaifa na matunda yalionekana kumpa wakati mgumu Mwingereza, aliyesalimu amri Desemba 9, 1961.

Hata baada ya Uhuru wa Tanganyika na baadaye Tanzania, Bibi Titi, alikuwa katika safu ya uongozi wa juu nchini kiserikali , huku akibaki alama na nembo ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), jumuiya inayodumu kuwa na nguvu ndani ya CCM ya leo, ikirithi majukumu ya TANU.


Hata leo Bibi Titi hajasahaulika, na katika kumuenzi mwanamama shujaa na jasiri wa Tanzania, vijana zaidi ya 3,500 kutoka mikoa ya Dar es Salaam na Pwani juzi walifanya matembezi ikiwa ni sehemu ya kumkumbuka Mama wa Taifa, kwenye njanja za kisiasa na kimaendeleo.

Matembezi hayo ya siku tatu yalianzia katika viwanja vya Mnazi Mmoja Dar es Salaam hadi Ikwiriri Rufiji Mkoa wa Pwani, yakiratibiwa na Taasisi ya Bega kwa Bega na Mama, anasema Katibu Mariam Amisi.

Wakiwa waandaji wa maadhimisho hayo ya Bibi Titi, anasema tukio linafanikishwa kwakushirikiana na wanachama wa klabu za kukimbia pamoja na waendesha bodaboda kufanya matembezi ya kuwaunga mkono Umoja wa Wanawake Tanzania (U.W.T).

"Matembezi haya yanajumuisha vijana 3,500 kati yao 500 wanatoka Pwani na waliungana na vijana wenzao katika mpaka wa Mkoa wa Dar es Salaam eneo la Kongowe," anasema Mariam.

Anaeleza kuwa baada ya kuondoka Kongowe yanaendelea katika Kijiji cha Mwarusembe wilayani Mkuranga, na kuendelea Kijiji cha Njopeka na Oktoba 21 na 22 watakuwa wamefika katika vijiji vya Bungu A na Kibiti mkoani Pwani.



Rais Nyerere alipokuwa na Bibi Titi Mohamed, katika nyendo zao za kisiasa, kabla ya uhuru wa Tanganyika na baada ya miaka mingi ya Muungano. **PICHA: MTANDAO.**

> "Matembezi haya yanajumuisha vijana 3,500 kati yao 500 wanatoka Pwani na waliungana na vijana wenzao katika mpaka wa Mkoa wa Dar es Salaam eneo la Kongowe," anasema Mariam.

Kadhalika, anaeleza kuwa matembezi hayo yataishia katika Kijiji cha Ikwiriri Wilaya ya Rufiji Oktoba 23, kutakuwa na shughuli mbalimbali zilizoandaliwa na UWT katika Uwanja wa Mashujaa.

Mariam anasema Bibi Titi Mohamed atabaki kuwa alama na nguzo muhimu ya mafanikio ya mwanamke hapa nchini.

**HISTORIA YAKE**

Mama wa Taifa, alizaliwa jijini Dar es Salaam Juni 1926, baba yake Mohamed Salim Mandwanga na mama yake Khadija Binti Salim, wote ni wenyeji wa Rufiji mkoa wa Pwani.

Bibi Titi Mohamed alifariki Novemba 5, 2000 nchini Afrika Kusini katika Hospitali ya Net Care, akiwa na miaka 74

Baba yake Bibi Titi alifariki wakati Titi akiwa na miaka tisa, hivyo baada ya kifo chake, mama yake alimpeleka shule kuanza masomo katika Shule ya Wasichana Kichwele ambayo leo inaitwa Uhuru.

Bibi Titi alimaliza elimu ya darasa la nne. Umaarufu wake katika siasa ulipata nguvu baada ya kuanzishwa kwa TANU, akishiriki katika mikutano mingi ya kisiasa na kijamii kuhamasisha harakati za uhuru na kuhimiza kujiletea maendeleo.

Bibi Titi ni miongoni mwa wanasiasa walioshuhudia kuunganishwa kwa African Association na Shiraz Association na kuzaliwa Afro Shiraz Party ya Zanzibar Februari 5, 1957

Katika miaka ya 1950, alikuwa ni miongoni mwa wanawake majasiri waliopigania uhuru wa Tanganyika kutoka ukoloni wa Mwingereza akiwa pamoja na Baba wa Taifa, chini ya chama cha TANU.

**UMAARUFU WAKE**

Bibi Titi alikuwa ni mwanamke wa kwanza kujiunga na harakati mbalimbali za kupigania uhuru wa Tanganyika na mwanzoni mwa harakati zake za kisiasa, alifanikiwa kulishawishi kundi kubwa la wanawake kujiunga pamoja kufikia mafanikio.

Akiwa kiongozi wa tawi la wanawake la chama cha TANU, Bibi Titi alikuwa na jukumu la kuwashawishi wanawake kuunga mkono maoni na sera za TANU.

Mwaka 1969, Bibi Titi alikabiliwa na rabsha za kisiasa na wenzake hata akaghafilika katika nyendo zake kashifa iliyomweka kando hadi mwaka 1977, alipopata msamaha wa Rais .

Baada ya hapo, aliishi maisha ya upweke bila ya familia yake wala marafiki zake aliokutana nao wakati wa harakati zake za kisiasa.

Ilipofika mwaka 1991 katika chapisho la chama la kuadhimisha miaka 30 ya Uhuru, Bibi Titi alitajwa kama "shujaa mwanamke' katika harakati za ukombozi". Moja ya barabara kuu jijini Dar es Salaam inatambuliwa kwa jina lake.



# HABARI DODOMA

## TARI yaagizwa kujenga kituo utafiti wa mazao

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (TARI) imetakiwa kujenga kituo cha utafiti wa mazao ya korosho, ufuta na karanga wilayani Kongwa mkoani Dodoma.

Hatua hiyo inalenga kuwasaidia na wakulima wa eneo hilo kukabiliana na kero mbalimbali ikiwamo upatikanaji wa mbegu bora na za kisasa ya mazao hayo.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema kwenye mkutano maalum wa wadau wa zao la korosho, wilayani Kongwa.

Alisema serikali itahakikisha inawasaidia wakulima wa zao hilo wanalima kisasa na kuuza korosho zao zikiwa zimebanguliwa.

"Naagiza Tari kujenga kituo cha utafiti kwa mazao ya korosho, ufuta na karanga katika eneo hili, pia kituo cha ubanguaji kitajengwa hapa, hii kazi ianze," alisema.

Aliwataka wakulima kulima mazao zaidi ya mawili katika mashamba ya mikorosho ili kupata kipato mwaka mzima.

Hata hivyo, alisema aliagiza Maafisa Ugani kuweka kalenda katika ofisi zao ili mkulima ajue miezi ya kupanda, kuweka dawa, kupalilia ni ipi huku akiahidi kuwa serikali inaangalia namna bora ya kuwapatia ruzuku.

Kwa upande wake, Spika wa Bunge na Mbunge wa Kongwa ambaye alikuwa Mwenyekiti wa mkutano huo, Job Ndugai, alisema zao hilo ni mkombozi katika wilaya hiyo na kwamba kinahitajika kiwanda cha kubangua korosho wilayani humo.

Alisema wakulima ni lazima waingie katika kilimo cha kisasa ikiwa ni pamoja na kuwa na simu janja ili kutatuliwa matatizo yao kwa wakati hususani miti inapokumbwa na magonjwa.

"Simu janja ni muhimu dunia ndio iko huko,unataka hutaki simu janja ni muhimu. Tumejipanga sasa Kusini mtupishe na iko siku tutawapa challenge," alisema Ndugai.

Naye Mkurugenzi wa Biashara na Masoko kutoka kampuni ya kusambaza viuatilifu ya Bens Agrostar Co Ltd, Patrick Mwalunenge, alisema wamekuwa wakitoa viuatilifu bora kwa wakulima wa zao hilo ambapo kwa sasa wamejipanga kuanza kufunga mabomba katika mashamba ya wakulima ili kukabiliana na magonjwa mbalimbali.

Aliwashauri wakulima kuwa na utaratibu kutibu magonjwa kwa wakati kwa kutumia dawa mbalimbali ambazo wanazo kwani mche wa mkorosho unahitaji matunzo ili uje utoa korosho bora.

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Mwema, alisema wamejipanga kuhakikisha zao la korosho linakuwa la kimkakati na linawasaidia wakulima kujiondoa katika lindi la umaskini.

Kadhalika, Ofisa Kilimo wa Mkoa wa Dodoma, Benard Abraham, alisema mikakati ya Mkoa wa Dodoma ni kutouza korosho ghafi na badala yake kila mkulima anatakiwa kubangua ili kujiongezea kipato.

# RC akataza upandishaji holela bei vifaa vya ujenzi

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewataka wafanyabiashara mkoani humo kutopandisha bei za bidhaa za ujenzi kiholela, hivyo kuwataka kuzingatia bei elekezi ya serikali.

Mtaka aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wafanyabiashara wa Dodoma kuhusu fedha za mkopo wa masharti nafuu zilizotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) wa Sh. trilioni 1.3 ambazo zimeelekezwa kwenye ujenzi wa miradi mbalimbali nchini.

Alisema fedha hizo zimegawanywa kwenye mikoa mbalimbali ili kutekeleza miradi ya ujenzi wa sekta ya afya, elimu na miundombinu kusaidia wafanyabiashara wadogo nchini ambapo Mkoa wa Dodoma umepata Sh. bilioni 17.97.

Mtaka alisema fedha hizo ni fursa kubwa kiuchumi kupitia biashara kwa kuwa zinakwenda kwa wafanyabiashara wazalendo wakati na wadogo ili kuwainua kiuchumi.

Alisema fedha hizo zimetolewa kwa lengo la kwenda kunufaisha sekta binafsi, wafanyabiashara wadogo na wakati, hivyo ni marufuku bidhaa za ujenzi kupanda bei kiholela.

"Naendapo ikatokea au kujulikana nyinyi wafanyabiashara mmepandisha bei kiholela, serikali ya mkoa itakwenda kununua bidhaa na vifaa vya ujenzi mikoa mingine," alisema Mtaka.

Aidha, alisema kupitia fedha hizo sekta binafsi inakwenda kukua na uchumi wa mtu mmoja mmoja kwa kuwa kila kata imepitiwa na ujenzi wa miradi ya maendeleo.

"Sasa niwaombe wafanyabiashara fedha zimetufikia sasa, tusilale tuchangamkieni soko hilo, masuala ya kulala unafungua duka saa sita mchana msije kumtafuta mchawi," alisema Mtaka.

Naye Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, alisema fedha hizo ni fursa kubwa kwenye uchumi kupitia biashara kwani zinakwenda kwa wafanyabiashara wazalendo wakati na wadogo.

"Nataka mtambue fursa zinazokuja lengo tunataka kuzalisha wafanyabiashara mamilionea na mabilionea kupitia fedha hizi, tunataka wafanyabiashara wadogo wakue na tubadilishe biashara zetu," alisema Prof. Mkumbo.

Kadhalika, Prof. Mkumbo aliwataka wafanyabiashara hao kuzingatia mambo makuu matatu ambayo ni pamoja na kutosheleza mahitaji.

Vilevile, alisema kuzingatia ubora kwa kuwa kumekuwapo na shida panapokuwa na mahitaji makubwa wafanyabiashara wamekuwa wakichukua bidhaa bila kuzingatia ubora.

"Tatu ni kuzingatia maadili ambapo wafanyabiashara wanatakiwa kusimama imara kwa kuuza bidhaa na kutoa stakabadhi tena ya mashine ya EFD," alisema.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya maridhiano mkoa wa Dodoma, Askofu Dk. Evance Lucas (aliyevaa suti nyeusi), akiwaongoza waumini huku wakiwa wameshika bendera ya taifa kuiombea nchi pamoja miradi ya maendeleo, kwenye ibada maalumu iliyofanyika mkoani humo, juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wasimamizi wa miradi watakiwa kuwa weledi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

JUMUIYA ya Maridhiano mkoani Dodoma imewataka wasimamizi wa miradi ya maendeleo ya serikali kuisimamia kwa weledi na kujiepusha rushwa na ubadhirifu wa mali.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo mkoani hapa, Askofu Dk. Evance Lucas, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye ibada maalumu ya maombi ya kuombea miradi mbalimbali inayotekelezwa na serikali iliyopo na itakayojitokeza kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Aliwataka wasimamizi wa miradi hiyo kuwa waaminifu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa la Tanzania kwa kujiepusha na vishawishi vya vitakavyokwamisha miradi hiyo.

Alisema kuwa serikali kupitia kwa Rais Samia Suluhu Hassan imefanikisha kushawishi Shirika la Fedha Duniani kutoa mkopo wa fedha Sh.trilioni 1.3 kwa ajili kuwezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mwenyekiti huyo alitaja baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa madarasa mapya 15,000 ya shule za sekondari na msingi 3,000, kutengeneza madawati 462,795 na ununuzi wa magari ya wagonjwa 395.

Aliwataka Watanzania kuhakikisha wanaiombea miradi hiyo ili ikamilike kwa wakati na kushauri viongozi wa dini kuhubiri amani na kuepuka ubaguzi wa kidini na kulinda nchi.

Alisema kuwa lengo la serikali ni kuboresha miundombinu katika sekta mbalimbali ili kuwasaidia wananchi kupata huduma za kijamii pamoja na maendeleo ya nchi, hivyo ni wajibu kwa kila Mtanzania kuombea miradi hiyo.



# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa mauaji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Mbeya, imemhukumu kunyongwa hadi kufa, Emmanuel Msomba (30) baada ya kupatikana na kosa la mauaji ya msafiri mmoja aliyekuwa akitoka Tunduma kwenda Sumbawanga mkoani Rukwa baada ya kumpiga na mti na kumpora fedha na simu ndogo aina ya Itel.

Uamuzi wa hukumu hiyo ulitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Mbeya, Zawadi Laizer, baada ya kusikiliza mashahidi zaidi ya wanane wa upande wa Jamhuri na kuridhika.

Hakimu Laizer alisema ushahidi huo ulieleza kwa kina kwamba mshtakiwa Msomba akiwa na wenzake wawili huko Kijiji cha Chiwanda, wilayani Momba, walimuua Isack Kazuka wakati akiendesha pikipiki kutoka Tunduma kwenda nyumbani kwao Kalambo, mkoani Rukwa.

Alifafanua kuwa marehemu Kazuka aliombwa lifti na mshtakiwa ambaye alishirikiana na wenzake kutekeleza mauaji hayo na kisha kumpora fedha na simu ndogo aina ya Itel baada ya pikipiki ya marehemu kudaiwa kuharibika.

Kwenye utetezi wake mshtakiwa Msomba alikana kutenda mauaji hayo badala yake alidai kuomba lifti ya pikipiki kwa Kazuka na aliachana naye kwa fundi wa pikipiki alikokuwa akitengeneza pikipiki yake hadi aliposikia mtu huyo amekutwa na umauti na kuiomba mahakama kumwachia huru kwa madai hakuhusika na mauaji hayo. Licha ya upande wa utetezi kuomba kupunguziwa adhabu wa mteja wake Jamhuri kupitia wakili Davice Msanga, kwenye utolewaji hukumu hiyo iliisihi mahakama kutoa adhabu kama sheria inavyoelekeza kwa kuwa bado watu wengi wanaendekeza uhalifu mbalimbali ikiwamo kukatisha maisha ya wenzao kwa tamaa za fedha na mali nyingine badala ya kufanya kazi kwa bidii na kumtanguliza Mungu.

Hakimu Mkazi Mfawidhi mkoa wa Mbeya, Zawadi Laizer kwa mamlaka ya nyongeza kutoka Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya baada ya kusikiliza mashauri ya mauaji, alimhukumu mtu huyo kwenda kunyongwa hadi kufa baada ya mahakama yake kuthibitishiwa mshtakiwa kumuua msamaria huyo aliyekatishwa maisha kijijini Chiwanda Momba wakati akielekea mkoani Rukwa.

Kwenye kesi hiyo mshtakiwa Msomba almaarufu Mnyiha (30) mnamo Oktoba 16, 2016, Kata ya Nkangamo wilayani Momba na wenzake wawili walimuua Isaack Kazuka kwa kumpiga na mti hadi kufariki kisha kumpora simu na fedha ambazo hazikutajwa kiasi kosa ambalo ni kinyume na kifungu namba 196 na kifungu namba 197 cha sheria ya kanuni za adhabu.



Baadhi ya wakazi wa Jiji la Mbeya, wakipata mahitaji katika Soko la Igawilo, jijini humo jana. Sado moja ya nyanya inauzwa 2,000/-. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## RC aomba NFRA kupunguza ununuzi mahindi Vwawa

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, ameuomba Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (NFRA), kupunguza ununuzi wa tani 400 za mahindi katika mji wa Vwawa na kuelekeza yanunuliwe katika Wilaya ya Mbozi.

Agizo hilo alilitoa jana baada ya kufanya ziara ya ghafla katika soko la mahindi Isongole.

Baada ya kufika katika soko hilo alibaini kuwapo shehena kubwa ya mahindi na kuagiza Wakala wa Hifadhi ya Chakula kuongeza tani za ununuzi kwenye wilaya hiyo.

"Wilaya hii ilipangiwa tani 800 za mahindi ndizo zinunuliwe, lakini kwa kuwa mahitaji ni mengi natoa maagizo haya, wakati serikali inaangalia namna ya kuhakikisha wakulima hawa wanapata soko la mahindi, nawaagiza NFRA kupunguza tani 400 ambazo mlipaswa kununua kwenye eneo la Vwawa mje mnunue huku kwa wakulima wa Isongole," alisema.

Kwa upande wao wakulima hao akiwamo Ubatizo Japioni na Mases Kayinga, waliishukuru serikali kwa kuamua kununua mahindi kwao, hata hivyo wakalalamikia hali ya soko kuwa bado ni changamoto kubwa na kuomba serikali kuongeza kiwango cha ununuzi.

"Mimi mwenyewe mahindi ninayo mengi sana hata hapa sijaleta kabisa, masoko hakuna kabisa tunaomba serikali itusaidie kupata masoko," alisema Japioni.

Katika msimu huu wa kilimo Mkoa wa Songwe ulizalisha mazao ya chakula tani milioni 1.4, wakati uhitaji ni tani 330,000 pekee na hivyo mkoa kubaki na ziada ya chakula ya tani zaidi ya milioni moja," alisema.

Hata hivyo, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, alitoa wito kwa wafanyabiashara nchini kwenda katika mkoa huo na kununua mazao na kuyauza nje ya nchi kwa kuwa tayari serikali ilishafungua milango ya kuuza nje ya nchi.

# Tanzania, Malawi kuendeleza ushirikiano wa kidiplomasia

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameahidi kuendeleza ushirikiano wa kidiplomasia na kibiashara baina ya Tanzania na Malawi kwa kutumia mpaka wa Kasumulu kuboresha mazingira ya utoaji wa huduma kwa wafanyabiashara na wananchi wanaozunguka eneo hilo.

Homera alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusu mafanikio yaliyopatikana baada ya ziara ya Naibu Waziri wa Ujenzi na Usafirishaji wa Malawi, Nancy Chaola, kufanya ziara mkoani Mbeya siku chache zilizopita. Alisema ziara hiyo imeleta matumaini ya kuongeza ushirikiano wa kibiashara baina ya Tanzania na Malawi kuzitumia kwa pamoja fursa zinazopatikana ikiwamo biashara ya mazao na bidhaa nyingine kulingana na mahitaji.

"Mtakumbuka tulipata ugeni wa kutembelewa na baadhi ya viongozi wa Malawi, tulijadili masuala mbalimbali ya ukuzaji uchumi na kufungua fursa mbalimbali za kibiashara kupitia mpaka wa Kasumulu nawahamasisha Wanambeya kuchangamkia fursa zinazopatikana," alisema Homera.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Ujenzi na Usafirishaji kutoka Malawi, alisema wanaendelea na jitihada za kuboresha miundombinu ya barabara, anga na reli ili kurahisisha shughuli za usafirishaji wa bidhaa baina ya nchi hizo.

Alisema amefurahishwa na utajiri wa rasilimali na hali nzuri ya hewa ambayo inafaa kwa mazao mbalimbali na miundombinu mizuri ya kusafirisha mazao na kwamba Malawi wamejipanga kutumia fursa hiyo. Katika ziara hiyo, Balozi wa Malawi nchini Tanzania, Glady Munthali, alisema watashirikiana na Serikali ya Tanzania kuhakikisha wafanyabiashara wa pande zote mbili wanafanya shughuli katika mazingira salama.

Vilevile, alisema wanaendelea kuhamasisha wakulima kulima mazao yenye ubora ili kukidhi mahitaji ya soko la dunia badala ya kuendelea kulalamika bila kuchukua hatua.



# Jamii yashauriwa umuhimu kunawa mikono

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

JAMII imeshauriwa kujenga tabia ya kunawa mikono ili kujikinga na maradhi ya miripuko ukiwamo ugonjwa wa corona na maradhi mengine ya maambukizi.

Hayo yalielezwa juzi na Ofisa Uongozi wa Taasisi ya Milele Foundation, Said Mtawa, wakati wa kilele cha Siku ya Kunawa Mikono Duniani kilichofanyika Shule ya Mbuyutende Matemwe, Wilaya ya Kaskazini 'A', Unguja.

Alisema sehemu kubwa ya jamii haijawa na mwamko wa kunawa mikono kama moja ya njia za kujikinga na maradhi mbalimbali yakiwamo ya kuambukiza badala yake hufanya hivyo yanapotokea maradhi jambo ambalo linapaswa kuepukwa. "Kwa mfano sasa hivi watu wananawa mikono kwa kuhofia kupata maradhi ya corona, lakini hawafanyi hivyo kama ni utamaduni wao," alisema Mtawa.

Alisema kunawa mikono kwa maji na sabuni kuna mchango mkubwa katika uimarishaji wa afya hasa za watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Mtawa alisema utafiti uliofanywa na Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) mwaka 2017, unaonyesha kwamba kuna upungufu wa miundombinu mizuri ya unawaji wa mikono kwa asilimia 70 majumbani, asilimia 84 ya shuleni na 47 ya vituo ya afya.

"Ili kukabiliana na maradhi ya corona, taasisi yetu ilitoa msaada wa vifaa vya kunawia mikono na kuihamasisha jamii kujenga utamaduni wa kunawa mikono kama njia ya kuepukana na maradhi ya kuambukiza," alisema.

Wakizungumzia umuhimu wa kunawa mikono, wanafunzi kutoka shule mbalimbali zilizoshiriki maadhimisho hayo, walisema kuna umuhimu wa kufanya hivyo ili kujikinga na maradhi.

Warda Makame Shaali wa Shule ya Mbuyutende, alisema awali hawakuwa na elimu ya umuhimu wa kunawa mikono, lakini baada ya kupatiwa elimu hiyo na kujengewa miundombinu ya kunawia waipa umuhimu. Mwanafunzi huyo aliwaomba wazazi na walezi kujenga tabia ya kunawa mikono watoto wao wanapotoka na kuingia nyumbani ili kujikinga na maradhi mbalimbali yakiwamo corona, matumbo ya kuharisha, kipindupindu na maradhi mengine ambayo huambukizika kwa kushikana.

Ofisa Afya wa Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja, Iliyasa Bakari Makame, alisema siku hiyo ni muhimu na ni ya kipekee kwa sababu inasaidia jamii kuona umhimu katika afya ya mwanadamu.

## Viongozi watakiwa kuwafichua watoro shuleni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI mbalimbali visiwani Zanzibar, wametakiwa kushirikiana hasa katika ngazi za shehia kwa kuwafichua watoto waliotoroka shule ili kuwarudisha kupata haki yao ya elimu.

Akizungumza jana katika kikao cha uhamasishaji wa mradi wa kuwarudisha watoto shuleni, Kaimu Katibu Tawala Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja, Mustafa Hassan Mkadam, alisema kumeonekana kuwapo vitendo vya udhalilishaji ambavyo vinaathiri kwa kiasi kikubwa watoto.

Alisema kwa mujibu wa taarifa alizozipata katika Mkoa wa Mjini Magharibi, kuna vijana 8801 ambao wametoroka shule ni imani yake baada ya kupata taarifa na maelekezo ya mradi huo watashirikiana kusaidia kuwarejesha watoto hao ili wapate elimu kwa maendeleo ya taifa.

Aliwataka washiriki wa kikao hicho kuyapokea vyema maelekezo watakayopatiwa na kuyatekeleza kwa vitendo na kuwa ni chachu ya kuleta mabadiliko kwa kuwaokoa watoto ambao ni tegemeo kubwa la taifa baadaye.

Naye Mkurugenzi Idara ya Elimu mbadala na watu wazima, Mashavu Ahmada Fakih, alisema kuanzishwa kwa mradi wa kuwarejesha watoto shule kutasaidia kupunguza watoto wa mitaani katika visiwa vya Zanzibar.

Alisema lengo la kikao hicho ni kuona kila mmoja ana wajibu wa kuwasaidia watoto hao ili wapate elimu ambayo itawasaidia kuondoa tatizo la watu wasiojua kusoma, kuhesabu na kuandika.

Mashavu alisema kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imedhamiria kuhakikisha watoto wote wanapata elimu ambayo itawasaidia katika maisha yao ya baadaye.

Alisema ni wajibu wa washiriki hao kuhakikisha wanatoa ushirikiano ili malengo ya serikali pamoja na mradi huo katika kuwapatia watoto elimu kufikiwa.

Kwa upande wake Mratibu wa Mradi huo, Mzee Shirazi Hassan, alisema mradi huo umeshaanza kutekelezwa na hadi sasa wamefanikiwa kuwarejesha shule watoto 2,600 kati ya 35,732 ambao hawakupata elimu na kuiomba jamii kushirikiana kwa lengo la kuwapatia elimu ambayo ni haki yao kikatiba.

Washiriki wa kikao hicho walisema wapo tayari kushirikiana na Wizara ya Elimu ili kufikia lengo la kuona kila mtoto ananufaika na elimu.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia), akiwa na viongozi mbalimbali katika sherehe za Maulid ya kuzaliwa Mtume Muhammad (SAW), katika viwanja vya Maisara Mjini Zanzibar juzi usiku. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waziri awaonya wanafunzi udanganyifu mitihani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Riziki Pembe Juma, amewahimiza wanafunzi wanaotarajiwa kufanya mitihani ya taifa, kusoma kwa bidii na kuacha tabia ya udanganyifu.

Alisema hayo katika Shule ya Donge Sekondari Mkoa wa Kaskazini Unguja, alipokuwa akizungumza na wanafunzi wa shule hiyo, ambao mwezi huu wanaratajiwa kufanya mitihani yao ya taifa.

Alisema siri ya kufaulu mitihani ni kusoma kwa bidii na si kufanya udanganyifu katika vyumba vya mitihani na kwamba ikibainika kuna athari kubwa ambazo mwanafunzi atakumbana nazo.

"Bado muda upo, kitu kikubwa kitakacho kuwezesheni kufaulu ni kuongeza bidii kwenye masomo, ukibainika kufanya udanganyifu katika chumba cha mitihani athari zake ni kutofikia malengo yako ya kimaisha," alisema.

Alisema dunia ya sasa inahitaji wasomi wa kada mbalimbali, wanafunzi lazima waelekeze nguvu zao katika elimu kwa kuwa ndiyo ufunguo wa maisha," alisema.

Alisema dunia imetanua wigo kutokana na maendeleo ya teknolojia, bila ya kuwa na elimu maana yake ni kuwekwa nyuma kwenye kila nyanja ya maendeleo.

Kwa upande wake, Mwalimu mkuu wa shule hiyo, Rajab Ali Salum, alimshukuru waziri huyo kwa ujio wake na kumhakikishia kuwa watajitahidi kadiri iwezekanavyo kufundisha kwa bidii na ubunifu kwa kuwajengea misingi imara wanafunzi wao kwa lengo la kupata ufaulu mzuri katika shule hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya wanakamati wenzake, Mwenyekiti wa kamati ya wazazi wa shule hiyo, Pili Ameir Machano, aliwataka wanafunzi hao kuwa makini wakati watakapoingia kwenye vyumba vya mitihani na kuelekeza nguzu zao zaidi katika elimu ili kupata ufaulu wa daraja la kwanza na kuijengea sifa shule hiyo.

Wakielezea changamoto zinazowakabili katika shule yao baadhi ya wanafunzi walisema wanakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa maji jambo ambalo linarudisha nyuma jitihada zao hasa katika kipindi hiki cha kuelekea mitihani na muda mwingi wanautumia wakiwa shuleni.

# SHAMRASHAMRA ZA SHEREHE YA MAULID



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akisalimiana na Sheikh Mkuu na Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi Bin Ally, wakati alipowasili katika viwanja vya Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera jana, wakati alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, kwenye Baraza la Maulid Kitaifa. **PICHA: OWM**



Baadhi ya waumini wa dini ya Kiislamu waliohudhuria Baraza la Maulid kitaifa, katika viwanja vya Kaitaba, Bukoba, mkoani Kagera jana. **PICHA: OWM**



Baadhi ya waumini wa dini ya Kiislam wa mkoa wa Dar es Salaam, wakiandamana kuadhimisha Maulid ya siku ya kuzaliwa Mtume Muhammad (SAW), katika Barabara ya Mtaa wa Lumumba, jijini humo juzi, wakiongozwa na Sheikh wa Mkoa huo, Alhad Mussa Salum (mwenye koti jeusi katikati). **PICHA: JUMANNE JUMA**




Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Maria Mwinyi (wapili kushoto), akiitikia dua ya Barzanji, wakati wa Maulid ya kusherehekea kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W) katika viwanja vya Maisara Suleiman, Wilaya ya Mjini Unguja juzi usiku. Kushoto kwake ni Mke wa Makamu wa Pili wa Rais, Mama Sharifa Omar Khalfan na Mke wa Makamu wa Kwanza wa Rais, Mama Zainab Kombo Shaib na (kulia kwake) ni Mke wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Mama Zuhura Kassim Ali. **PICHA: IKULU**



Wanafunzi wa Jumuiya ya Maulid ya Homu ya Mtendeni, Wilaya ya Mjini Unguja wakishiriki hafla ya Maulid katika viwanja vya Maisara Suleiman juzi usiku. **PICHA: IKULU**



Baadhi ya waumini wa dini ya Kiislamu wakiandamana Dar es Salaam jana kusherehekea Sikukuu ya Maulid. **PICHA: ANTHONY SIAME**

## Jeshi la Ethiopia lashambulia Mekelle

**Addis Ababa, ETTHIOPIA**

JESHI la Ethiopia limefanya shambulizi la anga dhidi ya raia katika mji mkuu wa mkoa wa Tigray, Mekelle.

Taarifa hizo ni kwa mujibu wa kikundi cha kisiasa ndani ya chama cha ukombozi wa watu wa Tigray, TPLF.

Watu watatu wamepoteza maisha na wengine kadhaa kujeruhiwa katika mashambulizi hayo ya mabomu.

Jeshi la anga la Ethiopia lilisema jana jioni kuwa limeshambulia mnara wa mawasiliano na vifaa, lakini likadai kuwa lilichukua tahadhari kubwa ya kuepuka madhara kwa raia.

Msemaji wa TPLF, Getachew Reda, aliandika kupitia ukurasa wa Twitter kwamba jeshi la anga lilituma ndege yake ya kivita kuwashambulia raia nje na ndani ya Mekelle, akiongeza kuwa Jumatatu huwa ni siku ya soko na hivyo kulikuwa na dhamira ya wazi.

Serikali ya Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, imekituhumu pia chama cha TPLF kwa kuwaua raia wapatao 30 kwa kutumia mizinga mikubwa.

**DW**

## Uganda yatengeneza gari la kwanza la kijeshi

**Kampala, UGANDA**

KAMANDA wa vikosi vya ardhi Uganda, Jenerali Muhoozi Kainerugaba, ameweka kwenye Twitter picha ya kile anachosema kuwa gari la kwanza la kivita kutengenezwa nchini humo.

Anasema liliundwa na kutengenezwa nchini Uganda, lakini hakutoa maelezo kuhusu muundo na gharama yake.

Gari hilo lililopewa jina la Chui, lilizinduliwa na baba yake, Rais Yoweri Museveni.

Jeshi la Uganda mwaka jana lilihusika katika msako mkali dhidi ya maandamano yaliyotikisa mji mkuu, Kampala, kufuatia kukamatwa kwa mgombea urais Bobi Wine.

Maofisa walitetea utumizi wa silaha za moto, wakisema polisi na jeshi walikuwa wakikabiliana na waandamanaji.

**BBC**

**Jeshi la Uganda mwaka jana lilihusika katika msako mkali dhidi ya maandamano yaliyotikisa mji mkuu, Kampala, kufuatia kukamatwa kwa mgombea urais Bobi Wine.**

# Vikosi DRC vyakabiliana na wanajeshi wa Rwanda

**Kivu Kaskazini, DRC**

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imesema kuwa vikosi vyake vimekabiliana na wenzao wa Rwanda karibu na mpaka wa Mashariki siku ya juzi.

Msemaji wa jeshi katika Mkoa wa Kivu Kaskazini alisema vikosi vya Rwanda vilivuka mpaka na kuingia Congo katika hatua ambayo ilisababisha makabiliano.

"Kitengo cha wanajeshi wa Rwanda kiliingia kilomita tano ndani ya Congo...hauwezi kuelezea jinsi wanajeshi waliojihami walivuka mpaka na kuanza kupiga risasi," Brigedia Jenerali Sylvain Ekenge aliiambia BBC Idhaa ya Maziwa Makuu.

Majeshi ya Rwanda hayajatoa tamko lolote kuhusu madai hayo au kujibu ombi la BBC.

Video zinazoshirikishwa mitandaoni zinawaonyesha wenyeji waliokuwa na hofu wakikimbia huku vikosi hivyo viwili vikikabiliana kwa rasasi. Wanajeshi wa Rwanda baadaye walirudi nyuma na kwenda nyumbani.

"Kwa bahati nzuri hakuna mtu aliyefariki katika tukio hilo," Jenerali Ekenge alisema.

Viongozi na wakazi wa eneo hilo walirejea majumbani mwao baada ya hali ya utulivu kudumishwa.

Mvutano wa mipaka kati ya majirani hao wawili wa Afrika Mashariki ni jambo la kawaida kwa sababu ya biashara haramu, ukosefu wa mipaka wazi na mashambulio ya waasi.

**BBC**



Mtoto akiwa amelala kwenye baiskeli akiendeshwa na baba yake wakikatiza mitaa ya mji wa Kabul, nchini Afghanistan, jana. **PICHA: REUTERS**

# Afrika yahitaji Dola bilioni 50 kukabili mabadiliko hali ya hewa kila mwaka

**New York, MAREKANI**

RIPOTI mpya inasema kuwa Afrika inahitaji hadi dola bilioni 50 kwa mwaka ili kukabiliana na tishio linaloongezeka la mabadiliko ya hali ya hewa.

Jumuiya ya Afrika na Shirika la Hali ya Hewa Duniani zinaonya kuwa karibu watu milioni 120 maskini, wanakabiliwa na tishio la mafuriko, ukame, makazi yao, na joto kali ifikapo mwishoni mwa muongo huu ikiwa hatua madhubuti hazitachukuliwa.

Pia inaonya kuwa barafu zilizosalia za barani Afrika ziko zinaelekea kutoweka ifikapo miaka ya 2040.

Afrika imeathiriwa na mabadiliko ya tabianchi ijapokuwa inawajibikia asilimia nne tu uzalishaji wa chafu duniani.

Pia, inaelezwa barafu adimu barani Afrika zitatoweka katika miongo miwili ijayo kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa, ripoti mpya ilionya.

Barafu adimu barani Afrika zitatoweka katika miongo miwili ijayo kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa, ripoti mpya ilionya jana wakati wa utabiri mkubwa wa maumivu kwa bara ambalo nchi zake zinachangia kwa kiwango cha chini kuongezeka kwa joto la ulimwengu lakini ndio zitaumia zaidi.

Mkutano mkuu wa Scotland ambao utaanza Oktoba 31, mwaka huu, ni ukumbusho mbaya kwamba watu bilioni 1.3 wa Afrika wanabaki hatarini sana wakati bara linapata joto zaidi, na kwa kiwango cha kasi zaidi kuliko wastani wa ulimwengu.

Wakati bado nchi 54 za Afrika zinawajibika kwa chini ya asilimia 4 ya uzalishaji wa gesi chafu duniani.

Ripoti hiyo mpya inamulika katika kupungua kwa barafu za Mlima Kilimanjaro, Mlima Kenya na Milima ya Rwenzori nchini Uganda kama ishara ya mabadiliko ya haraka na yaliyoenea yanayokuja.

Viwango vyao vya sasa vya kupungua ni vya juu kuliko wastani wa ulimwengu. Na ikiwa hii itaendelea, itasababisha kupungua kabisa katika miaka ya 2040, inasema ripooti hiyo.

**BBC/VOA**

HABARI MICHEZO

# KUIONA SIMBA, GALAXY KWA MKAPA BUKU TANO

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mabingwa wa nchi, Simba wakirejea juzi usiku, wakitokea Botswana kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy, tayari imeanika viingilio kuelekea mchezo wa marudiano utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili wiki hii.

Katika mchezo wa awali uliopigwa Uwanja wa Taifa wa Botswana Jumapili iliyopita, Simba iliibuka na ushindi wa mabao 2-0, hivyo inahitaji sare yoyote ama ushindi au kutokuruhusu kufungwa zaidi ya bao moja, ili kukata tiketi ya kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Licha ya Simba kupewa nafasi kubwa ya kutinga hatua ya makundi, hata kama ikitolewa na Jwaneng Galaxy, itaangukia kucheza mechi moja ya mtoano dhidi ya timu itakayopangiwa kutoka zinazoshiriki Kombe la Shirikisho Afrika, kuwania kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo ambayo ni ya pili kwa utajiri kwa ngazi la klabu barani Afrika.

Kuelekea mchezo huo, Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), limeiruhusu Simba kuingiza mashabiki 15,000 tu kutokana na ugonjwa wa COVID-19, ambao unaendelea kuitesa dunia kwa sasa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Klabu ya Simba, tiketi za mchezo huo tayari zimeshaanza kuuzwa kupitia mitandao yote ya simu ambapo mzunguko ni Sh. 5,000, VIP B na C Sh. 20,000 wakati VIP A ikiwa ni Sh. 40,000 tu.

Mbali na Simba, Azam FC na Biashara United pia zinaiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika na zitakuwa ugenini wiki hii kuwavaa wapinzani wao.

Azam FC ambayo ililazimishwa suluhu na Pyramids ya Misri, Jumamosi itashuka dimbani ugenini wakati Biashara United siku hiyo ikishuka uwanjani nchini Libya dhidi ya Al Ahli Tripoli.

Biashara United yenyewe itakuwa ikihitaji ushindi ama sare yoyote au kutokukubali kufungwa zaidi ya bao moja ili kusonga mbele baada ya mchezo wa awali uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Ijumaa iliyopita kushinda kwa mabao 2-0.

MSHINDI GOFU...




Victor Joseph (katikati), kutoka Dar es Salaam, akikabidhiwa kombe baada ya kuibuka mshindi wa jumla wa mashindano ya gofu yaliyofanyika katika viwanja vya Gymkhana jijini Arusha na kumalizika mapema wiki hii. **PICHA: TUMAINI MAFIE**

## Biashara United kuwafuata Walibya kesho

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha timu ya Biashara United kinatarajiwa kuondoka kesho, kuelekea Libya tayari kwa ajili ya mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF), dhidi ya wenyeji wao, Al Ahli Tripoli.

Wawakilishi hao wa Tanzania wanatarajia kucheza mchezo wa marudiano dhidi ya wenyeji wao hao, Al Ahli Tripoli, Jumamosi wiki hii, wakihitaji ushindi au sare yoyote ama kutokukubali kufungwa zaidi ya bao moja ili kusonga mbele baada ya mchezo wa awali katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kushinda 2-0.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwenyekiti wa Biashara United, Selemani Mataso, alisema taratibu za usafiri zinaendelea na timu yao inatarajia kuondoka kesho, Alhamisi kuelekea Libya tayari kwa mchezo wao wa marudiano. Alisema kuhusu idadi ya wachezaji watakaosafiri kwa mchezo huo itajulikana mapema kabla ya kuanza safari ya kuelekea Libya.

"Kila kitu kuhusu safari kinaenda vizuri, tunaendelea kuhakikisha timu inafanikiwa kwenda nchini Libya, kwa ajili ya kwenda kutafuta matokeo mazuri katika mchezo wetu huo wa marudiano," alisema Mataso.

Alisema uongozi unapambana kuhakikisha timu hiyo inafanikiwa kusafiri kwenda kucheza mechi hiyo ya marudiano na wanaimani kubwa ya kwenda kupata matokeo mazuri kwa kuwa Kocha wao, Patrick Odhiambo anaendelea na maandalizi ya mchezo huo.

"Tuna matarajio makubwa ya kwenda kufanya vizuri na kusonga mbele, tuna imani na wachezaji na kocha wetu, wanaenda kupambana kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri na kuweza kusonga mbele katika michuano hii," alisema Mataso.

## Masaka fiti Twiga ikiivaa Namibia leo

**Na Saada Akida**

TAARIFA njema imetua katika kikosi cha timu ya Taifa ya Wanawake ya Tanzania (Twiga Stars), ambayo leo itashuka dimbani dhidi ya Namibia kwenye mchezo wa kuwania kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (Afcon), baada ya kurejea kwa mshambuliaji wao hatari, Aisha Masaka.

Twiga Stars leo itashuka katika dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, kukabiliana na wapinzani wao, Namibia kusaka tiketi ya kufuzu fainali ya michuano hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime, alisema ni jambo la faraja baada ya mshambuliaji wao, Masaka kurejea kikosini na kuwa miongoni mwa wachezaji watakaokuwapo katika kikosi kitakachowavaa Namibia.

Alisema Masaka alikosekana katika michezo mitatu ya COSAFA, baada ya kuumia akiwa nchini Afrika Kusini, lakini sasa amepona na yuko katika mipango yake kuelekea mchezo huo muhimu kwao.

"Baada ya kutoka Afrika Kusini na Kombe la COSAFA, wachezaji walikuwa na furaha kubwa iliyonitia hofu nikihisi kwamba nitakuwa na kazi kubwa ya kuwasahaulisha ya Afrika Kusini.

"Hatimaye nimefanikiwa kuchukuwa muda mfupi kuwarejesha katika mstari na wote tumefanya kazi mapungufu yetu na ubora wa wapinzani wetu ili kuhakikisha tunafanya vizuri katika mchezo wetu wa kesho (leo) dhidi ya Namibia," alisema Shime.

Alisema wamefanya maandalizi mazuri na ana imani kurejea kwa Masaka kutaboresha kikosi chake katika safu ya ushambuliaji kwa kupata matokeo mazuri katika mchezo huo.

Tayari Kikosi cha Namibia kimewasili nchini tangu juzi mchana kwa ajili ya mchezo huo wa kuwania kufuzu Afcon.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SALAH ATAKA MPUNGA MREFU
MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 29, anataka mshahara wa karibu pauni 400,000 kwa wiki ili asaini mkataba mpya wa kuendelea kusalia hapo Anfield. **(Telegraph)**

### BEI YA SAVIC YATAJWA
LIVERPOOL imetaarifiwa na Lazio kwamba bei ya kiungo Mserbia, Sergej Milinkovic-Savic mwenye umri wa miaka 26, inaanzia pauni milioni 67. **(Calciomercato)**

### MAKOCHA KIBAO WATAJWA
KOCHA wa timu ya Taifa ya Ubelgiji, Roberto Martinez, kocha wa Rangers, Steven Gerrard na kocha wa Villarreal, Unai Emery wanatajwa kuwa kwenye orodha ya makocha wanaowaniwa kumrithi kocha Steve Bruce wa Newcastle United. **(Times)**

### ICARDI KUBADILISHWA NA AGUERO
KLABU ya Paris St-Germain huenda ikamtoa mshambuliaji wake, Mauro Icardi mwenye umri wa miaka 28, kubadilishana na mshambuliaji Sergio Aguero mwenye miaka 33 aliyejiunga na Barcelona akitokea Manchester City. **(El Nacional)**

### ARSENAL KWA ELYOUNOUSSI
ARSENAL na Leicester City zinamfuatilia winga wa Southampton na Norway, Mohamed Elyounoussi baada ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 kuonyesha kiwango bora tangu kuanza kwa msimu huu. **(Sun)**

### SOLSKJAER HAJAFURAHISHWA
KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer hajafurahishwa na klabu hiyo kushindwa kusajili kiungo katika dirisha lililopita la usajili. **(Manchester Evening News)**

### MBAPPE AGUSIA FURAHA
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, ambaye anawaniwa na Real Madrid, amegusia kwamba ana furaha PSG. **(Marca)**

### STERLING PAUNI MILIONI 80
KLABU ya Manchester City inataka euro milioni 80 kwa ajili ya mshambuliaji wake mwenye umri wa miaka 26, Raheem Sterling, ambaye anatakiwa na Barcelona. **(Marca)**

### BARKLEY AGOMBEWA ENGLAND
LEEDS United na Newcastle United zote zinamtaka kiungo wa zamani wa Chelsea na England, Ross Barkley mwenye umri wa miaka 27, ambaye anawaniwa na Burnley. **(90 Min)**

### ISAK AGOMBEWA MANCHESTER
MANCHESTER United itachuana na Manchester City katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Real Sociedad na Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 22. **(Fichajes)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ANCELOTTI: HUYU HAZARD SASA KACHANGANYIKIWA

**Amechoka kuendelea kuwa na matatizo haya, hajaumia, lakini kachoka sana...**

**BARCELONA, Hispania**

CARLO Ancelotti amedai hakuna mtu ambaye amechanganyikiwa kutokana na matatizo ya majeraha ya Eden Hazard kama mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji.

Hazard alijiunga na Real Madrid kutoka Chelsea mwaka 2019 kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 100, lakini nyota huyo wa zamani wa Blues amekumbana na majeraha tangu kuwasili kwake hapo kwenye mji mkuu wa Hispania.

Alicheza kwa dakika zote 90 kwenye mechi nne tu katika mashindano yote kwa Madrid, akifunga mabao matano katika mechi 51, hali iliyosababisha mashabiki na vyombo vya habari kumtolea macho mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30.

Ingawa Hazard ameanza katika mechi tano msimu huu akicheza nane kwa jumla ya dakika 382, lakini Ancelotti amethibitisha kwamba, nyota huyo atakosa mechi zaidi za Madrid.

Kukosekana kwa mchezaji huyo wa zamani wa Lille, Ancelotti amesisitiza kwamba Hazard amechanganyikiwa sana kutokana na matatizo ya majeruhi yanayomkumba.

"Hazard amechoka kuendelea kuwa na matatizo haya, hajaumia, lakini amechoka sana," alisema Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari, jana. "Hakuna mtu ambaye amechanganyikiwa kama Hazard. Nafikiri atakuwapo dhidi ya Barcelona au Osasuna."

Hazard amefunga bao moja tu na kutoa asisti moja katika dakika 799 alizoichezea Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya (akicheza mechi 12).

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 595

MECHI KALI
HOME
AWAY
MANCHESTER UTD
1.80 | 3.92 | 4.01
ATALANTA

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ARTETA AKERWA NA MWAMUZI DEAN



**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta alishangazwa na maamuzi ya mwamuzi Mike Dean kwa kushindwa kumtoa nje James McArthur wakati timu yake ikitoka sare ya mabao 2-2 na Crystal Palace kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, licha ya msaada wa VAR.

Alexandre Lacazette alifunga bao la kusawazisha dakika ya mwisho ya mchezo huo kuiwezesha Arsenal kupata pointi moja baada ya Palace kutoka nyuma ya bao 1-0 na kuongoza kwa 2-1, wakati kocha Patrick Vieira akirudi katika klabu yake hiyo ya zamani, Jumatatu.

Hata hivyo, Arteta anaamini Palace walitakiwa kupunguzwa na kubaki wachezaji 10 kabla ya mapumziko wakati McArthur alipomkanyaga Bukayo Saka mguu wa kushoto.

Licha ya tukio hilo, McArthur alionyeshwa kadi ya njano kutoka kwa mwamuzi Dean, wakati nyota huyo wa England, Saka akilazimika kutoendelea na mchezo huo kutokana na majeraha hayo.

Bosi huyo wa 'Washikabunduki', Arteta alikasirishwa na tukio hiyo na alitaka adhabu zaidi ingetolewa, hasa kwa usaidizi wa teknolojia ya video, VAR.

"Ilikuwa kadi nyekundu ya wazi kabisa. (McArthur) hakuwa na nia ya kupiga mpira," alisema akiiambia BBC Sport.

"Sijui VAR inafanyaje, hakutolewa nje."

Licha ya matokeo hayo, Arteta aliwasifia wachezaji wake kwa kuonyesha kiwango kizuri zaidi kwenye mchezo huo.

# Lewandowski mchezaji bora duniani - De Bruyne



**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa Manchester City, Kevin De Bruyne anaamini straika wa Bayern Munich, Robert Lewandowski ni mchezaji bora duniani.

Lewandowski ni mmoja wa wachezaji waliofunga mabao nane au zaidi kwenye mashindano yote katika ligi kubwa tano Ulaya msimu huu, akiwa na jumla ya mabao 15.

Nahodha huyo wa Poland amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi katika miaka ya hivi karibuni, akishinda mataji matatu na Bayern msimu wa 2019-20 na kuvunja rekodi ya Gerd Muller ya kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja wa Bundesliga, msimu uliopita.

Huku tuzo ya Ballon d'Or ikitarajiwa kutolewa mwezi ujao baada ya kuahirishwa mwaka jana, De Bruyne anahisi kiwango cha Lewandowski kwa kipindi cha miaka miwili hii kinamfanya awe anastahili kupewa tuzo hiyo.

"Ningependa kuangalia kipindi cha miaka miwili na ninamchagua Robert Lewandowski," alisema De Bruyne.

"Kwa kile alichokifanya kwa ufungaji mabao na kile alichoshinda pale Bayern Munich anastahili kabisa."

## HABARI MICHEZO

# 5,659,980

# JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/10/2021 | 17:00 | Leeds vs Wolverhampton | 2.33 | 3.41 | 3.01 |
| 02. 23/10/2021 | 17:00 | Millwall vs Stoke City | 2.37 | 3.16 | 2.97 |
| 03. 23/10/2021 | 17:00 | Peterborough vs QPR | 2.90 | 3.20 | 2.39 |
| 04. 23/10/2021 | 17:15 | Cadiz CF vs Alaves | 2.51 | 3.02 | 3.07 |
| 05. 23/10/2021 | 19:30 | Elche vs Espanyol | 2.71 | 3.02 | 2.82 |
| 06. 23/10/2021 | 22:00 | Athletic Bilbao vs Villarreal | 2.53 | 3.14 | 2.93 |
| 07. 24/10/2021 | 14:00 | Nice vs Lyon | 2.63 | 3.47 | 2.53 |
| 08. 24/10/2021 | 16:00 | West Ham vs Tottenham | 2.38 | 3.36 | 2.96 |
| 09. 24/10/2021 | 16:00 | Brentford vs Leicester | 2.62 | 3.27 | 2.72 |
| 10. 24/10/2021 | 17:15 | Barcelona vs Real Madrid | 2.65 | 3.54 | 2.53 |
| 11. 24/10/2021 | 18:30 | Stuttgart vs Union Berlin | 2.36 | 3.44 | 2.84 |
| 12. 24/10/2021 | 18:30 | Manchester Utd vs Liverpool | 3.07 | 3.62 | 2.21 |
| 13. 24/10/2021 | 19:00 | Roma vs Napoli | 2.62 | 3.43 | 2.62 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 20 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1229 | Vanraure Hachnohe FC vs Nagano Parceiro | 3.58 | 3.29 | 1.95 |
| 13:00 | 2181 | Ulsan Hyundai vs Pohang Steelers | 2.05 | 3.29 | 3.29 |
| 15:30 | 5670 | Albinoleffe vs Juventus U23 | 2.38 | 3.03 | 3.13 |
| 16:00 | 2949 | Kfum Oslo vs Bryne | 1.74 | 3.72 | 3.97 |
| 16:15 | 4265 | CA Rentistas vs CD Villa Espanola | 1.83 | 3.53 | 3.77 |
| 16:30 | 3853 | Golden Arrows vs Mamelodi Sundowns | 4.30 | 3.23 | 1.86 |
| 16:30 | 5818 | Pogon Grodzisk Mazowiecki vs Lech II Pozna | 2.65 | 3.30 | 2.65 |
| 17:30 | 1926 | Spartak Moscow vs Leicester | 4.21 | 3.56 | 1.85 |
| 18:00 | 2524 | FK Arsenal Dzerzhinsk vs Krumkachi | 2.60 | 3.50 | 2.55 |
| 18:00 | 5485 | HNK Rijeka vs Lokomotiva Zagreb | 1.58 | 3.96 | 4.73 |
| 18:30 | 3524 | Maritzburg Utd vs Orlando Pirates | 3.80 | 2.95 | 2.19 |
| 19:00 | 1270 | Fredrikstad vs Strommen | 1.30 | 5.02 | 7.73 |
| 19:00 | 2200 | KS Gornik Polkowice vs Puszcza Niepolomice | 2.11 | 3.15 | 3.29 |
| 19:00 | 3707 | Raufoss vs Stjordals-Blink | 1.55 | 4.09 | 4.87 |
| 19:00 | 4386 | Sandnes Ulf vs Aasane Fotball | 1.85 | 3.68 | 3.54 |
| 19:00 | 4947 | IK Start vs Grorud IL | 1.74 | 4.05 | 3.67 |
| 19:00 | 5165 | Ullensaker/Kisa vs Jerv | 3.19 | 3.53 | 2.01 |
| 19:00 | 5410 | Sogndal vs Ham-Kam | 2.66 | 3.48 | 2.31 |
| 19:45 | 4241 | RB Salzburg vs VfL Wolfsburg | 2.06 | 3.61 | 3.36 |
| 19:45 | 5281 | Barcelona vs Dynamo Kiev | 1.30 | 5.49 | 9.15 |
| 20:00 | 1199 | Valladolid vs UD Ibiza Eivissa | 1.73 | 3.44 | 4.82 |
| 20:00 | 1838 | La Serena vs Colo Colo | 6.20 | 4.07 | 1.45 |
| 20:00 | 2078 | Fuenlabrada vs Amorebieta | 1.57 | 3.46 | 6.72 |
| 20:00 | 3010 | AZ Picerno vs Nuova Monterosi | 2.47 | 2.93 | 3.08 |
| 20:30 | 5721 | Arsenal Sarandi vs Gimnasia y Esgrima | 2.71 | 2.91 | 2.62 |
| 21:00 | 1089 | Ranheim vs Aalesunds | 3.00 | 3.75 | 2.17 |
| 21:15 | 4514 | CA Fenix vs Liverpool (URU) | 3.85 | 3.85 | 1.85 |
| 21:30 | 5505 | OKS Odra Opole vs Skra Czestochowa | 1.99 | 3.28 | 3.48 |
| 21:30 | 5904 | Bari vs Foggia | 1.71 | 3.45 | 5.13 |
| 21:45 | 2027 | Middlesbrough vs Barnsley | 1.84 | 3.45 | 4.14 |
| 21:45 | 2083 | Fulham vs Cardiff | 1.49 | 4.25 | 5.92 |
| 21:45 | 2672 | Hull City vs Peterborough | 2.11 | 3.26 | 3.41 |
| 21:45 | 3241 | Preston vs Coventry | 2.66 | 3.16 | 2.61 |
| 21:45 | 4049 | Swansea vs West Bromwich | 3.91 | 3.16 | 1.99 |
| 21:45 | 4356 | Huddersfield vs Birmingham | 2.46 | 3.12 | 2.87 |
| 22:00 | 1532 | Alcorcon vs Leganes | 3.11 | 2.87 | 2.47 |
| 22:00 | 1554 | Taranto Sport vs Fidelis Andria | 2.34 | 3.10 | 3.20 |
| 22:00 | 1696 | Zenit St Petersburg vs Juventus | 3.40 | 3.11 | 2.25 |
| 22:00 | 2207 | Lugo vs Las Palmas UD | 3.50 | 2.96 | 2.22 |
| 22:00 | 2884 | Palermo vs Virtus Francavilla | 1.78 | 3.41 | 4.65 |
| 22:00 | 3482 | Latina vs Catanzaro | 4.10 | 3.50 | 1.88 |
| 22:00 | 3646 | BSC Young Boys vs Villarreal | 3.24 | 3.54 | 2.13 |
| 22:00 | 4264 | Lille vs Sevilla FC | 3.49 | 3.24 | 2.15 |
| 22:00 | 4554 | Catania vs Avellino | 1.99 | 3.25 | 3.95 |
| 22:00 | 4893 | Reading vs Blackpool | 2.14 | 3.30 | 3.30 |
| 22:00 | 5532 | Manchester Utd vs Atalanta | 1.80 | 3.92 | 4.01 |
| 22:00 | 5634 | Benfica vs Bayern Munchen | 6.81 | 5.01 | 1.40 |
| 22:00 | 5743 | Chelsea vs Malmo | 1.09 | 9.56 | 28.89 |
| 22:45 | 2440 | San Lorenzo vs Lanus | 2.76 | 3.24 | 2.36 |
| 23:30 | 1297 | Plaza Colonia CD vs River Plate (URU) | 2.17 | 3.38 | 2.95 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# INFANTINO NA KOMBE LA DUNIA KILA MIAKA MIWILI




**NYON, Uswisi**

RAIS wa Shirikisho la Soka duniani (FIFA), Gianni Infantino, ameelezea umuhimu wa Kombe la Dunia la wanaume na wanawake kufanyika kila baada ya miaka miwili.

Infantino amebainisha kwamba kumekuwa na ushirikishwa wa maoni kwa ndani ya chombo hicho na kwa pande zote zinazohusika kuhusu mpango huo na amesisitiza kuna faida nyingi zaidi chanya zitakazokuja kwa michuano hiyo kufanyika mara kwa mara.

"Tunachambua kama inawezekana kuandaa michuano ya Kombe la Dunia kila baada ya miaka miwili, kama itakuwa na faida chanya kwa soka letu," alisema Infantino Jumatatu akiwa kwenye Mji Mkuu wa Argentina, Buenos Aires.

"Kuna wazo hilo na sasa linafanyiwa kazi ndani na kutafuta ushauri kutoka pande zote. Kuna baadhi wanaunga mkono na wengine hawakubaliani na wazo hili."

Mpango wa Kombe la Dunia kufanyika kila baada ya miaka miwili unaoungwa mkono na Infantino, unapingwa vikali na Shirikisho la Soka la Ulaya (UEFA), Shirikisho la Soka la Amerika Kusini (CONMEBOL), Chama cha Klabu za Ulaya chenye timu 234, pamoja na Chama cha Wachezaji wa Kulipwa duniani (FIFPRO).

"Faida ya kuandaa michuano ya Kombe la Dunia kila baada ya miaka miwili inaonekana wazi kabisa kwa upande wangu," alisema Infantino.

Bara la Ulaya limeandaa michuano ya Kombe la Dunia mara 11, mara mbili zaidi kuliko bara lingine lolote.

Amerika Kusini limeandaa michuano hiyo mara tano, huku Afrika na Asia zikiandaa mara moja, na mwaka 2022 michuano hiyo itafanyika nchini Qatar.

# Koeman amtabiria makubwa Coutinho




**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Klabu ya Barcelona, Ronald Koeman, amemsifia kiungo, Philippe Coutinho baada ya kuonyesha kiwango bora katika ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Valencia, Jumapili.

Koeman amesema amekuwa akiamini katika uwezo wa mchezaji huyo na hafikiri atakuwa na majukumu makubwa katika timu hiyo siku zijazo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alisajiliwa Camp Nou akitokea Liverpool, lakini alishindwa kuonyesha ubora wake kutokana na majeraha ya mara kwa mara, Jumapili alifunga bao moja katika ushindi huo.

"Kilikuwa kiwango kizuri," alisema Koeman akiwaambia waandishi wa habari kwenye mkutano wake na wanahabari baada ya mechi alipoulizwa kuhusu kiwango alichoonyesha Coutinho na matokeo katika mchezo huo.

"Alipoingia kwenye mchezo alikuwa bora. Pamoja na uhuru wake tuliweza kudhibiti mchezo vizuri, anajua jinsi ya kufunga mabao.

"Amechukua hatua muhimu kwa sababu nimekuwa nikimwamini Coutinho. Kimwili, anazidi kuwa bora zaidi," aliongeza Koeman.

Michezo
Jumatano Oktoba 20, 2021
Nipashe



Ancelotti: Huyu Hazard sasa kachanganyikiwa

UKURASA 21

SIKU YANGU...




Kiungo wa Yanga, Feisal Sulum 'Fei Toto' (kulia), akishangilia pamoja na Jesus Moloko baada ya kuifungia timu yake bao la pili dhidi ya KMC FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Majimaji Songea jana na timu yao kuibuka na ushindi wa mabao 2-0. **PICHA: YANGA**

# YANGA NI MWENDO WA DOZI TU LIGI KUU

Yarudia rekodi ya msimu wa 2018/19, moto wa Fei Toto wazidi kuunguza KMC ikitepeta...

**Na Adam Fungamwango**

YANGA jana ilikwea juu ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kuiadhibu KMC mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Majimaji, Songea mkoani Ruvuma, ikiwa ni ushindi wa tatu mfululizo.

Kwenye mechi hiyo, imerudia rekodi yake ya msimu wa 2018/19, iliposhinda mechi tatu mfululizo za kwanza, ilipofungua dimba kwa kuichapa Mtibwa Sugar mabao 2-1, baadaye Stand United 4-3 na kisha Coastal Union bao 1-0.

Msimu huu ilianza kwa kushinda bao 1-0 kwenye mechi mbili dhidi ya Kagera Sugar na Geita Gold, kabla ya kuendeleza rekodi hiyo jana mjini Songea.

KMC kabla haijakaa sawa ilijikuta ikipachikwa bao dakika ya nne tu ya mchezo, likiwekwa nyavuni na Fiston Mayele, aliyeugusa mpira na kumpoteza maboya kipa Farouk Shikalo, ukitokana na shuti kali la Feisal Salum 'Fei Toto'.

Ilionekana kama vile wachezaji wa KMC wamechanganyikiwa baada ya bao hilo na haikushangaza walipofungwa lingine dakika sita baadaye.

Fei Toto kwa mara nyingine tena, akiwa hajakabwa na mchezaji yeyote, aliupata mpira kiasi cha mita 30, akavuta hatua moja na kuachia kombora kali, lililomwacha Shikalo akiruka bila mafanikio na 'ngoma' ikajaa wavuni.

Ilibidi benchi la ufundi la KMC lifanye mabadiliko dakika ya 29 tu ya mchezo kwa kumtoa Hassan Kapalata na kumwingiza Abdallah Masoud, baada ya kuona hali inakuwa mbaya.

Ni mabadiliko ambayo angalau yalileta ahueni kwa timu hiyo, kwani dakika moja baadaye ilifanya shambulizi kupitia kwa Hassan Kabunda, lakini shuti lake dhaifu lilidakwa na kipa Djigui Diarra, akiwa anadaka mpira kwa mara ya kwanza dakika ya 30.

KMC ikionekana sasa kuchangamka, ilifanya shambulizi lingine kali dakika ya 34, Kabunda alipoachia 'mashine' ya maana, lakini kipa Diarra 'alisafiri' na kupangua, ikawa kona ambayo nayo ilizua kizaazaa, lakini mpira ukatoka nje.

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko, lakini yaliifanya mechi ipooze zaidi kuliko kipindi cha kwanza na kama kawaida, Yanga ilionekana kupotea, wachezaji wake wakionekana kuchoka, ikiwa na tatizo linaloonekana ni la kudumu na halijapatiwa dawa.

Miraji Athumani, anayecheza kwa mkopo KMC akitokea Simba, angeweza kuipatia timu yake bao dakika moja baada ya mapumziko, alipobaki ana kwa ana na kipa Diarra, lakini kwa mshangao akapaisha mpira juu.

Mayele, mfungaji wa bao la kwanza, alishindwa kuukwamisha mpira wavuni dakika ya 61, alipomegewa pande kutoka kwa Djuma Shaaban, shuti lake likipiga nje ya nyavu akiwa anatazamana na kipa Shikalo.

Kipa Diarra alifanya kazi nzuri dakika ya 70, aliporuka na kupangua shuti la mbali, lililopigwa na mchezaji wa zamani wa Yanga, Kenny Ally na kuwa kona ambayo ilipigwa nje na Idd Kipagwile.

Kwa matokeo hayo, Yanga inafikisha pointi tisa, ikiwa na mabao manne, bila kuruhusu bao lolote mpaka sasa, ikiishusha KMC mkiani ikiwa na pointi moja tu, ikicheza mechi tatu bila kushinda hata moja.

## Simba yaanika siri ushindi Galaxy CAF

**Na Adam Fungamwango**

MSHAURI wa Mwekezaji wa Klabu ya Simba, Crescentius Magori, ameanika siri ya ushindi wa mabao 2-0, kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana na kuwataka wanachama na mashabiki wao kupuuza maneno ya baadhi ya watu kuwa ilikutana na timu mchekea.

Akizungumza baada ya kuwasili nchini wakitokea jijini Gaborone, Botswana juzi, Magori ambaye ni mshauri wa Mohamed Dewji, mwekezaji wa klabu hiyo, alisema Simba imepata matokeo mazuri kutokana ukweli kwamba kwa sasa wana uzoefu na michuano hiyo mikubwa ndani na nje ya uwanja, vinginevyo hali ingekuwa ngumu.

"Tulijiandaa na mechi ngumu. Na hii ni kwa sababu hivi sasa sisi ni wazoefu wa mashindano haya, haikuwa rahisi hata kidogo kama watu wanavyosema. Hii timu si mchekea kama watu wanavyodai, hivi majuzi kabla ya kucheza mechi yetu walicheza michezo miwili Afrika Kusini, wakatoka sare dhidi ya Mamelodi Sundowns na kufungwa bao 1-0 dhidi ya Orlando Pirates.

"Ni timu inayomilikiwa na kampuni ya mgodi wa almasi, wamesajili wachezaji wazuri, saba wanacheza timu ya Taifa ya Botswana na watatu ni wachezaji wa kigeni kutoka Afrika Kusini, kwa hiyo siyo timu ya mchezo mchezo," alisema Magori.

Alisema kilichotokea ni kwamba kwa sasa Simba ina wachezaji wazuri wenye uzoefu na ukomavu kwenye michezo ya kimataifa wakicheza ndani na nje ya nchi, lakini wao kama viongozi na makocha walijipanga madhubuti.

"Kocha aliisoma timu, tukapata mabao mawili ya haraka, alipanga mipango yake mizuri akalinda hadi mwisho. Mambo ya figisu huwa yanapunguzwa kama viongozi mkijipanga vizuri. Kuna watu walitangulia kwa ajili ya kuweka mambo sana. Na sisi pia tukafuata kabla timu haijawasili. Hii inaonyesha ni jinsi gani tulivyojipanga kukabiliana na mechi ngumu za kimataifa kama hizo," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >